# Nipashe

Jumamosi Novemba 7, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580392

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


**MAMBO** yazidi kuwa mabaya kwa Trump, familia yatoa neno

UKURASA 2



**MVUVI** asakwa kwa madai ya kumuua mgoniwe kwa kisu

UKURASA 4




UKURASA 11

# Uteuzi wa wabunge Viti Maalum waiva

**NEC** yamaliza kazi, majina kuwekwa hadharani wiki ijayo... *Endelea Uk. 2*



## Dk. Mwinyi ashtukia viashiria uvunjivu wa amani

UKURASA 3

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na waumini wa Dini ya Kiislamu baada ya swala ya Ijumaa, katika msikiti wa Nughe, jijini Dodoma jana. Aliwaomba wananchi na makundi yote kudumisha amani baada ya uchaguzi kuisha. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Ndugai , Tulia wapeta u-Spika, u-Naibu CCM

**ZUBEIR** Maulid aula tena uwakilishi Zanzibar...



UKURASA 2


SALAMU ZA PONGEZI



Gazeti Nipashe linampongeza Rais Dkt John Magufuli na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha Miaka 5. 2020 - 2025

Kwa salamu za pongezi
Wasiliana nasi kwa Simu: 0686 101335
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



SALAMU ZA PONGEZI

# John Ndugai, Tulia wapeta uteuzi CCM

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (NEC), imewateua kutetea nafasi zao aliyekuwa Spika wa Bunge la 11, Job Ndugai na Naibu wake, Dk. Tulia Ackson, baada ya kupitisha katika chekecheke vikao vya juu vya uamuzi.

Vilevile, NEC imetangaza siku tatu za vikao vya juu vya uamuzi kuwapitisha katika tanuru la mchujo kuanzia Novemba 16 hadi 18 mwaka huu, wanaoomba nafasi za umeya na uenyekiti wa halmashauri nchini.

Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (HKT) katika kikao chake maalum kilichofanyika juzi chini ya Mwenyekiti wake, Dk. John Magufuli.

Jana, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, alisema kikao cha kamati kuu ya halmashauri kuu ya taifa, kimepitisha majina hayo baada ya uchambuzi wa kina.

Alisema kuwa baada ya uchambuzi huo, ilipendekeza wanachama wa watakaosimama katika uchaguzi wa Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi.

Alisema Zuber Alli Maulid amependekezwa kugombea nafasi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi (BLW).

"Kamati kuu imekasimu kwa kamati maalumu ya taifa ukamilishaji wa mapendekezo ya kumpata Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi.

"Kamati kuu imetoa ratiba ya mapendekezo na uteuzi wa wagombea Meya/Wenyeviti/Makamu Wenyeviti wa Manispaa, Majiji, Halmashauri za Wilaya na Miji," Polepole alisema katika taarifa yake ya jana kwa umma. Kwa mujibu wa Polepole, kazi ya kuchambua na kuandaa taarifa kwa ajili ya kamati kuu juu ya wanaoomba nafasi ya kuteuliwa kugombea Meya wa Jiji, Manispaa na Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Miji, itaanza Novemba 16 na itamalizika Novemba 18 mwaka huu nchini ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

**PONGEZI KWA JPM**

Polepole alisema kuwa katika kikao chake, kamati kuu kwa kauli moja imempongeza Rais Dk. John Magufuli kwa kuchaguliwa tena kwa kishindo kilichovunja rekodi (asilimia 84.4) kuiongoa nchi yetu kwa muhula wa pili katika awamu ya tano.

# Uteuzi wabunge viti maalum waiva

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), inatarajia kukamilisha mchakato wa kuteua wabunge wa viti maalum na kutoa orodha yao wiki ijayo.

Imesema uteuzi huo unafanyika kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kisheria ikiwa ni pamoja na chama kutakiwa kupata walau asilimia tano ya kura halali za wabunge wote wa majimbo.

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, akizungumza na Nipashe iliyotaka kujua maendeleo ya mchakato huo jana, alisema tume itateua wabunge hao kulingana na orodha iliyowasilishwa na vyama husika.

Alisema orodha hiyo imewasilishwa na chama chenye sifa ya kupeleka ambacho kimepata asilimia tano ya kura halali za wabunge.

"Tunachoangalia ni idadi ya wabunge wote walioshiriki unajumlisha kura zao wote halafu ukimaliza unachukua asilimia tano ya kura za wabunge hao.

"Orodha (ya chama) inaletwa ikiwa imewapanga watu kuanzia mtu wa kwanza hadi wa mwisho na wengine wa ziada, kwa mfano una watu 10, unakuwa umeleta labda orodha ya watu 15," alifafanua.

Alisema kuwa kama chama kina sifa ya kupata wabunge watano wa viti maalum, kinawasilisha orodha ya wabunge 10 ambao wanakuwa wamepangwa kuanzia mtu wa kwanza hadi wa mwisho.

Mkurugenzi huyo alisema vigezo vingine vinavyoangaliwa ni vile vilivyopo kikatiba ikiwamo kuwa Mtanzania na kujua kusoma na kuandika.

Alisema sheria pia inakitaka chama kupanga wale wote wanaowataka kuanzia namba moja hadi ya mwisho.

"Kwa mfano, chama kina sifa ya kupata wabunge watano, wao wanakuwa wamewasilisha orodha ya wanaowataka kuanzia namba moja hadi 10, sasa ikitokea kwenye zile tano mmoja hayupo ndiyo anachukuliwa, anayefuata namba sita," alisema.

Alisema asilimia tano inapatikana kwa kuzingatia jumla ya kura zote zilizopatikana kwa wabunge wote walioshiriki uchaguzi kwenye majimbo 264 nchi nzima.

"Kwa mfano, umejumlisha umepata kura milioni 10, unachukua asilimia tano hizo, ndo unajua aah... unarudi sasa kwenye chama kile nacho wabunge wako zimefikia asilimia tano na kuendelea, kitakuwa na sifa ya kupata wabunge hao, kama hakina kitakuwa hakina sifa ya kupata nafasi hizo," alifafanua.

Alipoulizwa kama tayari tume imeshaainisha vyama vyenye sifa ya kupata wabunge wa viti maalum, mkurugenzi huyo alisema: "Ndiyo, lakini bado tupo kwenye vikao, na mchakato utakamilika wiki ijayo."

Katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28 mwaka huu, vyama vya upinzani viliambulia ushindi katika majimbo manane tu (mawili Tanzania Bara) kati ya 264 huku majimbo mengine yakichukuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) mabcho bila shaka kitakuwa na idadi kubwa pia ya wabunge wa viti maalum Bunge lijalo.



Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. John Magufuli, akiongoza kikao cha Kamati Kuu ya CCM, jijini Dodoma juzi.
**PICHA: IKULU**

# Mpinzani wa Donald Trump aimarishiwa ulinzi

**WASHINGTON, Marekani**

MGOMBEA Urais wa Marekani kwa tiketi ya Chama cha Democratic, Joe Biden (77), ameimarishiwa ulinzi kuanzia jana.

Biden ambaye pia ni Makamu wa zamani wa Rais, aliimarishiwa usalama kwa sababu huenda akatangazwa mshindi, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na gazeti la Washington.

Mgombea huyo katika uchaguzi mkuu wa Marekani uliofanyika Jumanne, hadi jana alikuwa akiongoza kwa kuwa na kura 253 dhidi ya mpinzani wake, Donald Trump ambaye alikuwa na kura 214.

Biden akishinda kura katika Jimbo la Pennsylvania au kwa kushinda majimbo mawili kati ya Georgia, Nevada na Arizona, atatangazwa kuwa mshindi katika nafasi hiyo ya urais.

Gazeti la Washington liliandika kuwa Biden ataongezwa idadi ya maofisa wa usalama baada ya timu yake ya kampeni kuiambia idara husika kwamba huenda angetoa hotuba muhimu jana.

Biden na timu yake ya kampeni wamekuwa katika kituo cha Wilmington, Delaware.

Wanaofuatilia uchaguzi kwa karibu pamoja na chombo cha habari cha CNN, walisema Georgia ambalo ni moja ya majimbo muhimu ambayo kura zake zilikuwa zikiendelea kuhesabiwa, Biden amechukua uongozi wa jimbo hilo kwa mara ya kwanza.

Msajili wa eneo la Clark katika Jimbo la Nevada, Joe Gloria, aliwaambia waandishi wa habari kuwa hawatamruhusu yeyote kuwazuia kutekeleza jukumu lao la kuhesabu kura.

Alisema maofisa wa usalama wamepelekwa eneo hilo na hatua zingine za kiusalama zikichukuliwa kuhakikisha wafanyakazi wako salama kuendelea na shughuli ya kuhesabu wa kura.

Gloria alisema masanduku ya mwisho ya kura yanayotarajiwa kuwasilishwa hapo baadaye huenda matokeo yakatolewa wiki ijayo kabla ya matokeo kamili kufahamika.

**WATOTO WA TRUMP**

Watoto wawili wa kiume wa Rais Trump, wamewashutumu wanachama wa Republican kwa kutomuunga mkono Rais anapokabiliwa na ushindani mkali kutetea muhula wa pili madarakani.

Mtoto mkubwa wa Trump, Don Jr, alikosoa chama kwa kuwa dhaifu.

Ndugu yake Eric alionya kwa kusema: "Wapigakura wetu hawatawahi kuwasahau, wakijifanya wanyonge."

Hatua hiyo inaashiria mgawanyiko ulioibuka kati ya washirika wa Trump ndani ya chama.

Ushindani mkali umeshuhudiwa huku Biden akionekana kuelekea kupata ushindi.

Trump ameapa kupinga matokeo ya uchaguzi huo mahakamani akitilia shaka shughuli ya kuhesabu kura inayoendeshwa akidai kumekuwa na visa vingi vya udanganyifu.

Wanasiasa wa ngazi ya juu katika chama cha Republican kama vile Seneta wa Utah, Mitt Romney na Gavana wa Maryland, Larry Hogan wameonya hatua ya kuhujumu mchakato wa kidemokrasia.

Profesa wa Sheria katika Chuo Kikuu cha Southampton, Jacob Eisler, aliliambisha Shirika la BBC Radio 5 Live, kuwa kesi zilizowasilishwa na kampeni ya Trump ni dhaifu.

Eisley alisema kuwa ana wasiwasi kwamba Trump huenda akang'ang'ania madarakani.

"Kile kinachomshinikiza kufanya hivyo (Trump) ni maslahi yake binafsi," alisema.

"Trump ana fursa ya kukabiliana na mtihani huu huku akiendelea kuwa na ushawishi mkubwa katika chama cha Republican."

**BBC**

## HABARI KITAIFA

# Mwinyi abaini viashiria uvunjifu wa amani



**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (pichani), amesema uchaguzi mkuu umemalizika salama lakini kuna viashiria vidogo vidogo vya uvunjifu wa amani.

Kutokana na hali hiyo, amewataka Watanzania kukataa vitendo hivyo na kudumisha amani iliyopo ili kupata maendeleo zaidi kwa wananchi wote wa Tanzania.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipopata nafasi ya kutoa neno la shukrani kwa waumini baada ya kusali sala ya Ijumaa kwenye Msikiti wa Nunge, jijini hapa ambao alikuwa akiutumia kusali kabla ya kuwa Rais.

Alisema uchaguzi umefanyika kwa amani na usalama, hivyo jukumu lililo mbele yao ni kudumisha amani.

"Wosia ninaotaka kutoa leo hapa ni kujitahidi sote kwa pamoja tuhakikishe tunailinda amani tuliyo nayo. Maimamu na Masheikh katika misikiti wahubiri amani, sisi wanasiasa popote tulipo tuhubiri amani, na kila mwananchi ahakikishe anailinda amani," alisema.

Rais Mwinyi alisema bila amani hakuna kitakachofanyika si maendeleo ya nchi wala ibada.

"Kwa hiyo amani ndiyo kitu cha kwanza na mengine yatafuata. Tumemaliza salama uchaguzi lakini vipo viashiria vidogo vidogo vya kutaka kuvunja amani iliyopo. Sote kwa umoja wetu tukatae na tudumishe amani yetu na Mungu atatujalia kupata maendeleo zaidi," alisema.

"Mustakabali wa nchi yetu unategemea amani tuliyo nayo, tabia ya binadamu haoni jambo kama lina umuhimu mpaka limwondoke. Kuthamani kitu ulicho nacho inakuwa vigumu hadi ukikosa. Hata afya tulizo nazo kila siku ukiamka mzima huoni umuhimu wa afya, siku utakayoumwa ndiyo utajua kumbe afya ni muhimu," alisisitiza.

Dk.Mwinyi alisema katika suala la amani hakuna nafasi ya kujaribu.

"Itoshe yale tunayoyaona kwenye vyombo vya habari katika nchi mbalimbali kama vile Syria, Iran, Yemen na Somalia na nyingine zisizo za Kiislam, amani ikishavunjika kusali pamoja kama namna hii haiwezekani," alisema.

"Mchakato umeisha awamu ya kwanza ilikuwa ni kupata nafasi nimeshaipata nashukuru Mungu, awamu inayofuata ni kuwatumikia watu lakini jukumu lililopo mbele yetu ambalo ni kubwa na zito linahitaji dua, niombeeni niwatumikie watu kwa uadilifu na kwa haki," alisema.

Aliwashukuru waumini wa msikiti huo kwa kumuombea kwenye uchaguzi huo.

Naye Imamu wa Msikiti huo, Abdi Mussa, alisema Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, mzee Ali Hassan Mwinyi, ambaye ni baba wa Dk. Mwinyi, alipewa kuwa Imamu wa Msikiti huo kwa hiyo kwa sasa wanampa cheo hicho Rais Dk. Mwinyi.

Alimpongeza Rais huyo kwa kuchaguliwa kuiongoza Zanzibar na kuahidi kuwa waumini wa msikiti huo na wananchi wa Dodoma kwa ujumla, wataendelea kumwombea kwa Mungu ili ampe hekima na busara katika kuwaongoza wananchi.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

**Anwani ya Simu: "Uvuvi"**
**Simu Nambari: +255 (026) 2322612**
**Nukushi: +255 (026) 2322613**
**Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz**
**Tovuti: http://www.mifugouvuvi.go.tz**

**Mji wa Serikali Mtumba,**
**Mtaa wa Ulinzi,**
**S.L.P 2847,**
**40487 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

### KUFUNGULIWA KWA MSIMU WA UVUVI WA KAMBAMITI (PRAWNS) KWA MSIMU WA MWAKA 2021

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inapenda kuwatangazia Kampuni na wananchi wote kwamba, uvuvi wa Kambamiti (Prawns) kwa msimu wa mwaka 2021 utafunguliwa tarehe 1 Machi hadi tarehe 30 Septemba, 2021 kwa Kanda ya Kaskazini (Dar Es Salaam, Tanga, Bagamoyo na Saadani). Aidha, uvuvi huo kwa Kanda ya Kusini (Kisiju, Rufiji delta, Jaja/Kilwa, Lindi na Mtwara) utafunguliwa tarehe 01 Aprili hadi tarehe 31 Agosti, 2021.

Kwa tangazo hili, kila kampuni au mwananchi mwenye nia ya kufanya uvuvi wa kambamiti kwa msimu wa mwaka 2021, anaombwa kutuma maombi kuanzia tarehe 10 hadi tarehe 30 Novemba, 2020. Waombaji wanapaswa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003, Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 na Marekebisho yake ya Mwaka 2020. Aidha, vigezo vya kuzingatia katika maombi ya uvuvi tajwa vinapatikana katika Tovuti ya Wizara (www.mifugouvuvi.go.tz) na katika Ofisi za Wizara Kanda ya Dar Es Salaam na Pwani.

Maombi ya leseni za uvuvi wa Kambamiti kwa wavuvi wadogo yatumwe katika Halmashauri husika na wavuvi wakubwa yatumwe kwa Katibu Mkuu - Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**Imetolewa na:**

**DKt. Rashid A. Tamatamah**
**KATIBU MKUU - UVUVI**

HABARI KITAIFA

## Mbuzi watajwa mauaji ya mke

**Na Waandishi Wetu,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshirikia Boshu Kulwa (60) kwa tuhuma za kumuua mkewe, Magidalena Lunguya (45) kwa kosa la kuhoji uuzwaji wa mbuzi wa watoto wake.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nyamingu yalikotokea mauaji hayo, Masesa Manyanda, alisema jana kuwa tukio lililokea majira ya saa tisa alfajiri ya Novemba 5, mwaka huu huko katika Kijiji cha Nyamingu, Kata ya Busangi, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama.

Alisema kuwa siku ya tukio, alifuatwa na watoto watatu wa marehemu wakidai baba yao amempiga na kuumua mama yao, hivyo akafuatana nao kwenda nyumbani kwa marehemu na kukuta mama amekufa akiwa amelazwa chumbani akiwa na majeraha mwilini, sikio la kushoto likiwa limekatwa na kitu chenye ncha kali.

Manyanda alidai chanzo cha tukio hilo ni mama huyo kuhoji mume wake kuuza mbuzi ambaye ni mali ya watoto kwa Sh. 15,000 na kufidiwa mbuzi mdogo na mnunuzi bila kujua matumizi ya fedha hizo.

Alisema kuwa baada ya chakula, walikwenda kulala na majira ya saa tisa usiku kuliibuka mzozo mkubwa baina ya wanandoa hao na majirani walisikia sauti ya marehemu akilia kwa muda mfupi kisha kukawa na ukimya.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, watoto waliamka na kwenda kuangalia kilichotokea na kukuta mama yao amenguka chini huku damu zikiwa zinatapakaa chumbani.

Manyanda alisema kuwa, baada ya kubaini tukio hilo, alitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kata na Jeshi la Polisi Busangi ambao walifika katika eneo la tukio na kumchukua mtuhumiwa kwa ajili ya taratibu nyingine za kisheria.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, akibainisha kuwa tayari ameshamwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Msalala kufuatilia suala hilo.

# Asakwa tuhuma kumuua mgoni wake

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi mkoani Lindi, linaMSAKA mkazi wa mji mdogo wa Kivinje, Juma Ngozi (25), maarufu kama Hamorapa, kwa tuhuma za kumuua anayedaiwa kuwa mgoni wake, Abdallah Raisi.

Ngozi anadaiwa kumuua baada ya kumtuhumu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mchumba wake, Sharifa Mpunga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Stanley Kulyamo, alisema jana kuwa alisema mauaji hayo yalitokea mwanzoni mwa wiki iliyopita.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni Ngozi kukuta kwenye simu ya mchumba wake ujumbe ukimwelekeza mahali pa kukutana na Raisi.

"Nyumbani kwa wachumba hawa kwa muda mrefu kumekuwa na mtafaruku wa kutokuwa na maelewano mazuri. Waliwahi kusuluhishwa na wazazi bila mafanikio," alisema Kulyamo.

Kamanda huyo alisema kutokana na ujumbe huo, Ngozi ambaye ni mvuvi, alimweleza mchumba wake huyo ampeleke safari yake na asilipotekeleza atamweka kwenye orodha ya kuondoa uhai wake, amri ambayo Sharifa aliitii.

Akasema walipofika eneo ambalo Raisi walikubaliana kukutana na sharifa ili kutekeleza kile walichokikusudia, akiwa ameketi juu ya pikipiki yake akimsubiri mpenzi wake huyo, mtuhumiwa alichomoa kisu na kumshambulia maeneo mbalimbali ya mwili na kuondoa uhai wake.

Kamanda Kulyamo alisema wakati Ngozi akitekeleza mauaji hayo, mchumba wake alitimua mbio kwenda kituo cha Polisi kujisalimisha kwa kuwa naye alikuwa miongoni mwa waliotakiwa kuuawa na mtuhumiwa huyo.

Mtuhumiwa baada ya kutekeleza mauaji hayo, alisema alichukua pikipiki ya marehemu na kuondoka nayo kusikojulikana na kwamba wanaendelea kumtafuta ili afikishwe kwenye vyombo vya sheria kujibu mashitaka yanayomkabili.

Katika tukio lingine, polisi wanamsaka mkazi na mkulima wa Kijiji cha Chimbira 'A', wilayani Ruangwa, Fantalion Weva, kwa tuhuma za kumuua mke wake, Letisia Ng'ombo (44) kwa kile kinachodaiwa ni wivu wa mapenzi.

Kamanda Kulyamo alisema Weva anadaiwa kufanya mauaji hayo wiki iliyopita nyumbani kwao, cha Chimbira 'A' kwa kumkata mkewe koromeo kwa kutumia kitu chenye ncha kali na kusababisha kifo chake.

Kulyamo alisema chanzo cha mauwaji hayo ni wivu wa kipenzi baada ya kumshukuru mkewe kuwa na mahusiano wa kimapenzi na mwanamume mwingine, hali iliyompandisha hasira mtuhumiwa kutekeleza mauaji hayo. Alisema Weva alitekeleza mauaji hayo wakati mkewe akiwa amelala usingizi ndani ya nyumba yao, ndipo alipochukua kitu chenye ncha kali na kumkata koromeo.

"Huyu mtuhumiwa baada ya kumwona mkewe amelala usingizi, alichukua kitu chenye ncha kali na kumchoma shingoni," alisema ACP Kulyamo.

Pia alisema mtuhumiwa baada ya kufanya kitendo hicho, alitoroka kijijini hapo na kwenda kusikojulikana. Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka ili kumkamata na kumfikisha katika vyombo vya sheria.



Diwani Mteule wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (kulia), akikagua mradi wa maji katika soko la samaki la kimataifa la Magogoni maarufu Feri, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maofisa mawasiliano maji wasisitizwa ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**

MAOFISA mawasiliano wa sekta ya maji wametakiwa kuwa wabunifu wanapotekeleza majukumu yao na kuhakikisha wanauhabarisha umma kuhusu masuala mbalimbali yahusuyo maji.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, kwa niaba ya Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, alipokuwa akifunga kikao kazi cha maofisa mawasiliano wa sekta ya maji mkoani Singida.

"Ninatoa wito, muwe wabunifu, mwende na wakati, muandike makala katika vyombo vya habari na majarida na mutangaze Wizara kwa umma ikiwa katika taswira chanya," alisema.

Mhandisi Kemikimba aliwataka maofisa hao kutobweteka kwa kusubiri vyombo vya habari vitangaze kuhusu sekta hiyo kisha waanze kujibu hoja zilizotolewa.

Badala yake aliwataka wahakikishe wanauhabarisha umma kwa wakati kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Habari ya mwaka 2016, inayowataka kutoa habari kwa wananchi.

Aidha, Mhandisi Kemikimba aliwaagiza maofisa hao kuhakikisha wanaifahamu vyema sekta nzima ya maji kwa ukamillifu ili kutekeleza ipasavyo jukumu la kuitangaza vizuri.

Sambamba na hilo, aliwataka kujitathmini kwa kuangalia endapo katika maeneo yao ya kazi wananchi wanapata huduma ya maji na kuangalia miradi inayotekelezwa katika maeneo hayo endapo inafanya kazi na kushauriana na watendaji wao namna bora ya kuitangaza miradi hiyo.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Masoko, Chuo cha Maji, Ghanima Chanzi. alisema kikao kazi hicho kitamsaidia kuboresha utendaji kazi.

"Ujuzi huu utaniwezesha kuhakikisha jamii inatambua chuo cha Maji kinafanya majukumu gani ya msingi katika Sekta ya maji mathalani katika kuzalisha wataalamu wa sekta ya maji," alisema.

Lengo la kikao hicho pamoja na masuala mengine, lilikuwa kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi pamoja na kupata mafunzo juu ya masuala muhimu yanayohusu wajibu wa maafisa mawasiliano, matumizi ya mitandao ya kama njia ya mawasiliano, utifaki, anuai za jamii na umuhimu wa rasilimali za maji.

TANGAZO

IPP



# Salamu Za Pongezi

Mh. Dkt. John Pombe Magufuli & Mh. Samia Suluhu Hassan

Uongozi na wafanyakazi wa kampuni za **IPP** wanaungana na Watanzania wote kumpongeza Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuongoza tena Serikali ya awamu ya tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .

***Hongera sana.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji Simba,Yanga wapeni furaha mashabiki

**WATANI** wa jadi nchini, Yanga na Simba wanatarajia kukutana katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2020/21 utakaochezwa kuanzia saa 11:00 jioni leo kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Mechi hiyo ya raundi ya saba ni ya kiporo, awali mchezo huo ulipangwa kufanyika Oktoba 18, mwaka huu lakini kwa sababu zilizokuwa nje ya uwezo wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi (TPLB), ulisogezwa mbele.

Hatimaye siku hiyo nyingine imefika na vigogo hao wa soka nchini, timu zote kutoka Kariakoo jijini, zinakutana na kila upande ukiwa na rekodi yake tofauti, tangu kuanza kwa msimu huu wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18, kutoka mikoa mbalimbali.

Yanga yenye pointi 23 na inayofundishwa na Mrundi Cedric Kaze, ndio mwenyeji wa mchezo huo dhidi ya mabingwa watetezi, Simba ambao wana pointi 19 mkononi na wanaonolewa na Mbelgiji Sven Vandenbroeck. Mechi ya watani wa jadi imekuwa ikivutia idadi kubwa ya mashabiki wa soka na wadau wa michezo walioko ndani na nje ya Tanzania. Ni mchezo ambao umekuwa maarufu katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na vile vile umeshaingia kwenye rekodi za Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kutokana na kushuhudiwa na mashabiki wengi, ikitajwa ni moja ya 'dabi' chache ambazo zinaendelea kutikisa kwenye bara hili. Ili mechi hiyo iendelee kuwa na heshima na mvuto, ni wakati wa wachezaji wa Simba na Yanga kuonyesha ubora wao kwa kucheza kandanda la kiwango cha juu ambalo linatarajiwa na mashabiki na wanachama wao.

Klabu zote mbili zilisajili wachezaji wapya na kuimarisha mabenchi ya ufundi, si tu kwa malengo ya kufanya vyema kwenye msimu huu, lakini wakiangalia ushindi pale wanapokutana.

Inaelezwa na imekuwa ikionekana ni bora Simba na Yanga wafungwe na klabu nyingine, lakini si kufungana wenyewe wanapokutana. Mashabiki, wanachama na viongozi wanaeleza hupata maumivu sana pale mmoja anapofungwa na mwenzake na machungu hayo hayamalizika mpaka watakapokutana katika mchezo mwingine.

Kufanya vizuri kwa wachezaji katika mechi ya leo, si tu kutaipa timu yake ushindi, lakini pia kutawaongezea thamani nyota husika kwa kupewa au kuboreshwa mikataba yao huku pia wakiwavutia mawakala wa nje ambao watafuatilia mchezo huo.

Kuonyesha kiwango kizuri, nidhamu pia kutawapa nafasi ya nyota hao kuitwa na vile vile kupata namba kwenye vikosi vya timu za mataifa wanayotoka.

Mbali na wachezaji kuonyesha kandanda la kufurahisha, Nipashe inawakumbusha waamuzi waliopewa jukumu la kuchezesha mchezo huo kufanya uamuzi wa haki kwa wakati wote.

Uamuzi wa haki utawajengea heshima waamuzi husika na vile vile utasaidia timu iliyofanya vizuri kupata ushindi na si ile ambayo itaonekana au kusemekana imebebwa na wasimamizi hao wenye dhamana ya kuamua kwa kupiga filimbi yao.


Hii pia itasaidia waamuzi hao kuendelea na majukumu yao na si kuifanya Kamati ya Saa 72 kuwafungia, uamuzi ambao hautaunifaisha timu iliyoonewa, lakini vile vile makosa yatakayofanyika yatasababisha waamuzi husika kupotea kwenye medani ya kazi hiyo waliyoichagua. Nipashe pia linapenda kuwakumbusha mashabiki watakaoingia uwanjani kuwa watulivu wakati wote na kufahamu haki waliyonayo ni ya kushangilia tu na kuacha tabia ya kuwapiga waamuzi pale wanapoona wanaonewa.

Mashabiki wanatakiwa kufahamu TFF imeweka wasimamizi wa mchezo huo, na waamini kila ambaye ataenda kinyume na kanuni zilizowekwa, atachukuliwa hatua na hii itasaidia kuhakikisha mechi hiyo inachezwa bila ya upendeleo. Vitendo vya uharibifu wa mali vinavyofanya na mashabiki viepukwe au matukio ya kupigana yasipewe nafasi katika mchezo huu wa leo ambao mshindi atakuwa amejiweka kwenye nafasi nzuri ya kusogea kileleni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga, Simba leo ni leo



Na Barnabas Maro

**"LEO** ni leo, asemaye kesho ni mwongo." Mambo ya leo yanapaswa kufanywa leo, anayesema yasubiri hadi kesho ni mwongo.

Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam, leo utaamua mbabe kati ya mahasimu (watu wanaochukiana, wapinzani katika kandanda, maadui) wawili, yaani Yanga na Simba ingawa wanaitwa 'watani wa jadi.'

Kwa kawaida watani hawachukiani wala kutukanana na kuhasimiana. Yanga na Simba hufanyiana mambo hayo. Kamwe huo si utani.

Uwanja wa Benjamin Mkapa hautakuwa na sinema wala riwaya bali ni mchezo upendwao sana duniani wenye majina mengi: kabumbu, soka, kandanda na gozi. Wengine husema 'gozi la ng'ombe nyama kala nani.'

Milango ya uwanja itakuwa wazi kuanzia mapema asubuhi, Yanga ikiwa mwenyeji wa Simba kwenye mzunguko wa saba wa pambano la Ligi Kuu ya Tanzania Bara itakayochezwa kuanzia saa 11:00 jioni.

Ni mchezo utakaokata ngebe yaani maneno yasiyo na maana, maneno mengi yenye jeuri na majigambo yatolewayo na mashabiki wa pande zote mbili.

Kwa mpangilio (kuweka mambo au vitu kwa kufuata utaratibu uliowekwa), mpaka sasa Azam ndiyo inayoongoza kwa alama 25 baada ya kucheza mechi 10 ikifuatiwa na Yanga iliyocheza mechi tisa ikiwa na alama 23 huku mabingwa watetezi, Simba ambayo nayo imecheza mechi tisa ikiwa na alama 19.

Simba ilimalizia hasira zake kwa Mwadui baada ya kupoteza michezo miwili mfululizo. Kwanza ilifungwa bao moja na Tanzania Prisons kule Sumbawanga kisha mechi iliyofuata ikafungwa tena bao moja na Ruvu Shooting jijini Bandari ya Salama!

Nachelea kueleza tambo za msemaji wa Ruvu Shooting. Nani asiyemfahamu Masau Bwire kwa tambo zake timu yake inapozishinda Simba na Yanga?

Chelea ni neno lenye maana tatu: kwanza ni kipande cha mti mkavu kinachofungwa kwenye wavu ili wavu uelee. Pili ni kitendo cha kutofanya jambo kwa kuhofia madhara yake; -wa na hofu ya, -wa na wasiwasi wa. Maana ya tatu ya neno hilo ni teremka.

Suala la Bwire linahusu maana ya pili ya neno 'chelea.' Usiombe timu yako ifungwe na Ruvu Shooting kwani waweza kupata mshituko wa moyo kwa maneno na tambo za Bwire. Nawaachia wenye meno watafune ila mimi simo!

Kwa upande mwingine, Yanga waliokuwa wageni wa Gwambina FC walitoka suluhu ya bila kufungana hivyo kuwa na sare mbili, tofauti na Simba na Azam zeye sare moja kila moja.

Ushauri wangu kwa wanachama na mashabiki wa Yanga na Simba ni huu ufuatao: "Kusifiwa si kuona, shani* ni kujionea." *Shani ni jambo au kitu cha kushangaza yaani kioja.

Maana yake hata ukasifiwa jambo vipi na mtu aliyeshuhudia haiwi sawa na kujionea mwenyewe. Huwa heri kulishuhudia jambo wewe mwenyewe badala ya kutegemea kuelezwa na walioliona au waliolishuhudia.

Kwa maana nyingine, kusikia sio kuona. Yaani kusifiwa si kuona, shani ni kujionea. Nendeni uwanjani ila kwa wenye maradhi ya moyo wasiende ili wajiepushe kuanguka uwanjani na kuzirai!

Huu ni ushauri wangu kwani huo uwanja wa Benjamin Mkapa nausikia tu kwa jina na kuuona kwenye runinga ingawa nimekuwa 'raia' wa Bandari ya Salama tangu mwaka 1960 nikiwa mwandishi wa gazeti maarufu kwa habari za 'pembe za chaki' lililoitwa 'Ngurumo.'

Onyo lililotolewa mapema la watazamaji kutokwenda uwanjani na silaha ya aina yoyote lafaa kuzingatiwa sana. Baadhi ya watazamaji huingia uwanjani na silaha huku wakiwa wamelewa chicha (hali ya kulewa sana; chordo, chopi, chakari.)

Uwanja wa michezo si wa vita bali ni uwanja wa burudani yaani hali ya mtu kufarijika kutokana na kupata au kuona kitu anachokipenda hivyo wasiende wakiwa wamelewa.

Kadhalika ile tabia ya kuwatukana wachezaji na watazamaji wa upande mwingine isiwepo abadan (kukataa au kukanusha uwezekano wa kutokea jambo; asilani!)

Kufanya hivyo ni uhuni yaani tabia zisizopendeza. Watazamaji huenda kwenye viwanja vya michezo kujiburudisha si kusikia matusi wala kupigana.

Jambo lingine ni tahadhari kwa waamuzi (marefarii) watakaochezesha mechi hiyo inayosubiriwa kwa hamu kubwa nchini kote na kwingineko wanakofuatilia kwa makini ushindani wa Yanga na Simba. Wachezeshe kwa haki bila upendeleo.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## TASAF sasa kuzifikia kaya maskini mil. 1.4

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Mpango wa kunusuru Kaya Maskini kipindi cha pili cha awamu ya tatu unatarajia kuzifikia zaidi ya kaya 1,407,154 Tanzania Bara na Zanzibar.

Mkurugenzi wa Programu za Jamii wa TASAF, Amadeus Kamagenge, alisema hayo hivi karibu jijini Tanga wakati wa kikao kazi cha kujenga uelewa kuhusu mpango wa kunusuru Kaya maskini (PSSN II), kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Unguja na Pemba.

Kamagenge alisema katika kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF kinachotekelezwa kuanzia mwaka 2020 hadi 2023, kaya 1,407,154 zimelengwa.

Alisema utekelezaji utafanyika kwenye halmashauri 185 za Tanzania Bara na Unguja na Pemba ikiwa ni pamoja na asilimia 30 ya vijiji, mitaa na shehia ambazo hazikufikiwa kwenye utekelezaji wa kipindi cha kwanza ambazo hazikuandikishwa .

Kamagenge alisema madhumuni ya mpango wakati wa kipindi cha pili awamu ya tatu ni kuwezesha kaya za walengwa kutumia fursa za kuongeza kipato, huduma za jamii uchumi na kuwekeza katika kuendeleza watoto wao ili kuleta matokeo chanya yatakayodumu kwa muda mrefu kwenye kaya hizo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema mpango wa kipindi cha pili cha awamu ya tatu, gharama za utekelezaji wake ni dola za Kimarekani milioni 883. 31 ( sawa na Sh. trilioni 2.05) ambazo ni wastani wa asilimia 0.5 ya pato la taifa.

Mwamanga alisema Februari 17, mwaka huu, Rais John Magufuli alishafanya uzinduzi wa kuashirikia utekelezaji uanze kufanyika.

Alisema tayari utekelezaji wa awamu ya tatu umeanza kufanyika kwa kutia saini hati ya makubaliano baina ya halmashauri zote, sekretarieti za mikoa ya Tanzania Bara na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar .

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Judica Omari, katika hotuba yake ya ufunguzi, aliwataka waandishi wa habari kutumia kalamu zao kuandika kwa usahihi habari za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kwenye utekeleaji wa kipindi cha pili awamu ya tatu ya mfuko huo ili kuepuka upotoshaji.

# Wazazi wapewa somo kuwaepusha watoto wa kike vitendo vya ukatili

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

JAMII na wazazi wametakiwa kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa watoto ili kuwanusuru na vitendo vya ukatili, mimba za utotoni zitakazochangia kukatisha masomo na kutofikia ndoto zao.

Wito huo ulitolewa jana na Meneja Mipango wa Shirika la Wadada Solution on Gender Based Violence, Anitha Samson, katika mkutano wa viongozi wa kijamii na wadau mbalimbali juu ya uhamasishaji wa huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana na kupinga vitendo vya ukatili.

Alisema elimu ya afya ya uzazi ni nguzo imara kwa ustawi wa jamii hivyo kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kuhakikisha huduma rafiki za afya za uzazi kwa vijana zinapatikana sambamba na elimu sahihi.

"Kuna wadau mbalimbali kama walimu, polisi wote wanashughulika na vijana lakini tatizo kubwa ni vijana kutokupata taarifa sahihi hivyo ni wakati wa kuwapa elimu hasa ya uzazi ambayo ndio msingi mkubwa katika maisha yao lengo likiwa ni kuhakikisha tunaishi katika jamii salama bila ukatili na mazingira salama hususani watoto wa kike ambao ndio kundi kubwa linaloathirika,"alisema Samson.

Revina Theognance, Mkuu wa Upelelezi wa Polisi (OC-CID) Wilaya ya Kwimba, alisema wazazi wasichoke kuwalea watoto kwa kuwa kumekuwa na tabia ya kuwapeleka watoto wadogo shule za bweni na wasiwapeleke kwa bibi bali wawalee wenyewe ili kuwaepusha na vitendo vya ukatili, pia aliwataka walimu nao wasichoke kuwafundisha kwani muda mwingi ndio wanashinda nao.

"Kila mmoja aguswe na mtoto tujitahidi kuhakikisha mtoto wa Tanzania ndoto zake zinatimizwa na kufika pale panapotakiwa hivyo ni vyema wazazi wavunje ukimya na kutochoka majukumu yao," alisema Theognance.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto Jiji la Mwanza, Bertha Yohana, alisema idadi kubwa ya vijana walio katika balehe, hujihusisha na vitendo vya ngono isiyo salama.

Kwa mujibu wa takwimu za Watu na Hali ya Afya ya mwaka 2010 ( TDHS 2010) vijana wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kujihusisha na vitendo vya kujamiiana.

Alisema takwimu hizo zinaonesha kuwa wasichana wengi huanza kujihusisha na ngono wakiwa na umri wa miaka 18, ambao ni asilimia 59 wakati wavulana huanza wakiwa na miaka 20 ambao ni asilimia 45.

Pia alisema takwimu hizo zinaeleza kuwa wasichana kati ya umri wa miaka 15-24, sawa na asilimia 13 wameshajamiiana kwenye umri wa miaka 15 kulinganisha na asilimia saba kwa wavulana.

Alisema ili kupunguza na hatimaye kuwaondolea vijana matatizo hayo, kila kiongozi wa serikali, dini na mashirika yasiyo ya kiserikali katika ngazi zote, anapaswa kutetea sera za kuboresha huduma za afya ya uzazi kwa vijana, kutetea na kuokoa maisha ya vijana kwa kuboresha afya uzazi kwa kundi hilo pamoja na kuweka matatizo ya vijana kuwa ni agenda muhimu katika shughuli zao kila siku.

Naye Mkuu wa Polisi (OCD) Wilaya ya Ilemela, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi Elisante Ulomi, alisema kushamiri kwa vitendo hivyo kumesitisha ndoto za wanafunzi ambao wengi wao wanaambulia ujauzito wakiwa shuleni.

" Pia ipo tabia ambayo inasumbua ambayo ni kutokuwepo kwa ufatiliaji kwa wazazi ,wengine kwa kushirikiana na watoto wao udiliki kujadiliana na mlengwa ili kumaliza kesi hivyo kesi ikifika mahakamani mashahidi hawafiki kutoa ushahidi" anaeleza Ulomi

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Polisi Wilaya ya Ilemela Inspekta Hilda Maleko, alisema wanafanya jitihada za kulikomboa kundi hilo kwa kupita mashuleni na kutoa elimu kuhusu afya ya uzazi ukatili, mimba za utotoni na kuwaeleza madhara ya kujihusisha na mapenzi katika umri mdogo na umuhimu wa elimu ya afya ya uzazi.



Kijana akishusha barafu kutoka kwenye gari kwa ajili ya kuhifadhia samaki katika soko la samaki la kimataifa la Magogoni, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# CRDB yazindua kampeni ya kuhamasisha wananchi

**Na Nelson Simon,** SAUT

BENKI ya CRDB imezindua kampeni ya 'Tupo Mtaani Kwako' inayolenga kuhamasisha matumizi ya huduma za kibenki na kuwaunganisha Watanzania walio wengi kutumia huduma zake.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Biashara Mkuu wa Benki hiyo, Dk. Joseph Witts, alisema kampeni hiyo itasaidia kuelimisha wateja juu ya fursa mbalimbali wanazozitoa.

"Tuna jukumu la kuhakikisha tunasaidia kuboresha maisha ya Watanzania kupitia bidhaa na huduma zetu na kampeni hii tunakwenda kutimiza wajibu huu kwa kutembelea mtaa kwa mtaa Tanzania nzima kuhakikisha wananufaika na fursa zinazotolewa na CRDB," alisema.

Dk. Witts alisema CRDB imejipanga kuwatembelea wateja waliko ofisini, sokoni, dukani, stendi na kuwapatia huduma.

"Tutakuwa tukitumia magari na mabango ambayo tutayaweka mtaani kwa ajili ya kusogeza huduma kwa wateja," alisema.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo inalenga kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utoaji huduma ikiwamo CRDB Wakala, SimBanking, TemboCard na InternetBanking.

Alisema kupitia njia hizo, mteja anaweza kufanya miamala yake ya kibenki popote alipo kwa urahisi, usalama na unafuu.

Meneja wa Kanda ya Mashariki ya Benki ya CRDB, Badru Idd, aliwataka Watanzania kuchangamkia fursa hiyo na kuahidi kuwa benki hiyo imejipanga kikamilifu kuhakikisha inamfikia kila mtu.

"Tunaanza na Kanda ya Mashariki ambayo inajumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar na baadaye kusambaa nchi nzima. Niwaombe Watanzania wanapoona wafanyakazi wetu mtaani, wasisite kuuliza maswali na kuja kupata huduma, hii ni benki yao na tupo tayari kuwahudumia," alisema.

## Wanachama NSSF kunufaika na NHIF

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANACHAMA wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Kahama mkoani Shinyanga, waliojiandikisha na kuchangia ipasavyo, wanatarajia kunufaika na matibabu kupitia Mfumo wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Akizungumza juzi na waandishi wa habari ofisini kwake, Meneja wa NSSF Mkoa wa Kahama, Aisha Nyemba, alisema watakaonufaika na mfuko huo ni wale walijiunga na kuchangia michango kwa miezi sita mfululizo.

Nyemba alisema wananchama waliojiandikisha na kuchangia Sh. 20,000 kwa miezi sita na kuendelea, wanatarajia kunufaika na mfuko wa matibabu bure kupitia NHIF huku wanaochangiwa na waajiri wao wakinufaika na matibabu bure na si mima ya afya.

Pia alisema kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo kuanzia Julai, mwaka huu, walitarajia kuwasajili wanachama wapya 150 lakini wamesajili 68 pekee na hao wakichangia vyema michango, watakuwa miongoni mwa wanachama wanaokwenda kunufaika na NHIF.

"Wachimbaji wadogo ni wagumu kujiunga na NSSF licha ya kuwaeleza muhimu wa mfuko ambavyo atanufaika hapo baadaye. Hivi karibuni tutakwenda kuzungumza na wachimbaji wadogo katika machimbo madogo ya Mwime Ilindi ili nao wajiunge," alisema.

Nyemba aliwataka wanachama wote wanaochangia wenyewe kila mwezi kuhakikisha wanatoa michango hiyo kwa wakati na si kusubiri mpaka wakumbushwe ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wenzao kujiunga na NSSF kwa faida ya uzeeni.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki na Waendesha Pikipiki na Bajaji Mkoa wa Shinyanga (CHAWADAP), Idsam Mapande, alisema amekuwa akishirikiana na NSSF katika kuwahamasisha waendesha pikipiki na bajaji kujiunga na mfuko huo.

Pia alisema vijana wanaoendesha bajaji na bodaboda wengi wamekuwa wakipata ajali mara kwa mara na kushindwa kumudu gharama za matibabu kutokana na ukosefu wa fedha na wengi wamejiunga na mfuko na badhi yao wanaendelea kunufaika na NSSF.

Naye Amos Ben, Dreva bodaboda kituo kikubwa cha mabasi mjini hapa, alisema bado hajajiunga na mfuko huo kwa kuwa hajapata elimu ya namna ya kujiunga na kunufaika na kwamba akipewa elimu atajiunga na kuwahamasisha wenzake pia kujiunga.

# TARA kuwezesha upimaji bure saratani

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Waradiografia Tanzania (TARA), kimesema kitatatoa huduma za vipimo bure, ikiwamo upimaji wa saratani ya matiti pamoja na tezi dume, Novemba 8, mwaka huu.

Katibu wa chama hicho, Mradiolojia Omary Msehwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, akizungumza na Nipashe, kuhusu maadhimisho ya siku ya waradiografia duniani inayofanyika Novemba 8, kila mwaka.

Alisema chama hicho ambacho kinajumuisha wataalamu wa sonografia, radiografia na radiotherapi watatoa huduma hiyo katika hosp[itali za Raditech Polyclinic zilizopo Ilala na Temeke, jijini.

"Siku hii ni kumbukumbu duniani ya mgunduzi wa huduma ya X-ray, Prof. Wilhelm Conrad Roentgen mwaka 1895. Katika maadhimisho ya mwaka huu, Novemba 8, tutatoa huduma ya vipimo bure, kumuona mtaalamu bure, kuanzia saa 2 asubuhi hadi 11 jioni.

Lengo ni kuwafikia watu wazima kuanzia umri wa miaka 40 hadi 45, wanawake tutawapima saratani ya matiti na wanaume tezi dume, kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia kama ultra sound, hii fursa nzuri sababu wataalamu wa radiografia watakuwepo," alisema Msehwa.

Pia alisema ujumbe wa mwaka huu kati maadhimisho hayo ni kuboresha huduma za afya kwa kutumia vifaa vyenye teknolojia, kutaongeza kasi ya ugunduzi wa maradhi na upatikanaji wa tiba.

Siku hiyo huadhimishwa Novemba 8, kila mwaka ili kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu tiba ya vifaa vya kiteknolojia ambavyo husaidia upatikanaji wa matibabu.




Meneja Biashara wa Tigo, Suleiman Bushagama, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, katika hafla ya kuwazawadia washindi wa awamu ya kwanza ya kampeni inayoendelea ya Jaza Tukujaze Tena. Kulia ni Balozi wa kampeni hiyo, Meena Ally. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wadogo watahadharishwa masika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo mkoani Shinyanga, wametakiwa kuchukua tahadhari ya kuangukiwa na kifusi cha udongo wakati wakiendelea na shughuli za uchimbaji wa madini kwa kipindi cha mvua za masika licha ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kutangaza kutakuwa na mvua chache.

Mhandisi Joseph Kumburu, Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, alitoa tahadhari hiyo jana alipozungumza na Nipashe kwa njia ya simu. Alisema upungufu wa maji utaongezeka ya kutumia kwenye shughuli za uchakataji wa madini.

"Kama mnavyojua, tuko katika vipindi vya mvua za masika, hivyo utabiri wa hali ya hewa unaonyesha kuwa baadhi ya maeneo yanatarajia kupata kiwango cha mvua za chini za wastani. Hali hii pia inaweza kusababisha madhara makubwa kwenye sekta ya madini," alisema Kumburu.

Pia Kumburu alisema kukosekana kwa mvua kutasababisha kuwa na upungufu mkubwa wa maji katika shughuli za madini na ajali ya kuangukiwa na ukuta hasa wakati mvua zinaponyesha, hivyo wachimbaji wanatakiwa kuchukua tahadhari kwa kujenga vyema maduara yao licha yakuwa na mvua chache.

Alisema magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu yataongezeka kutokana na uchafu na miundombinu ya migodi na mazingira yataharibika na kuwataka wachimbaji kuzingatia utunzaji na matumizi sahihi ya maji ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

Pia aliwataka viongozi na wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini kuzingatia sheria na kanuni za usalama za uchimbaji wa madini ikiwa ni pamoja na kusitisha shughuli za uchimbaji katika maduara wakati wa mvua inaponyesha. Aliwasisitiza kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduara na kuhakikisha maduara yote yamefungwa na kuyafunika ili kuzuia maji kuingia ndani ya maduara wakati wachimbaji wakiendelea na shughuli za uchimbaji wa madini.



# Aahidi kupeleka wabunge wote JKT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MGOMBEA uspika katika Bunge lijalo, David Ndiege, amesema kama atachaguliwa kuliongoza bunge la 12, atahakikisha wabunge wote wanapelekwa kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kujengewa misingi ya uzalendo.

Ndiege aliyasema hayo jana wakati akizungumzia nia yake ya kutaka kuwa Spika wa Bunge la 12 linalotarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni na Rais John Magufuli.

Alisema akiwa Spika wa Bunge la 12, atahakikisha anamwomba Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uzalaendo wabunge wote.

Kwa mujibu wa Ndiege, ana imani kuwa mafunzo hayo yatawafanya wabunge kujitambua na kuzingatia kile ambacho kimewapeleka bungeni na kuacha mizaha na mambo mengine yasiyofaa kama ambavyo wengi wamekuwa wakifanya.

"Lakini pia katika uongozi wangu, nitahakikisha naliongoza Bunge kwa misingi ya utawala wa kidemokrasia ambao utakuwa unazingatia kanuni za Bunge kwakua hakuna kitu kinachoweza kwenda bila ya kuwepo kwa kanuni," alisema.

Kabla ya kuanza kwa vikao vya Bunge, alisema ataiomba kutoa mafunzo ya kubadili mienendo ya tabia za wabunge ili wajitambue na kufanya kazi ya kuisaidia serikali lakini pia kuikosoa.

Vilevile alisema kama Bunge litakuwa halina nidhamu, serikali haitafanikiwa kutekeleza majukumu yake kwani muhimili huo ndiyo sehemu pekee ya kuisaidia serikali.

"Pia nitahakikisha bunge linakuwa na kitengo cha ukaguzi wa ndani wa fedha za mfuko wa jimbo ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha hizo kwa wabunge na kusaidia wananchi kunufaika nazo," alisema Ndiege.

Kuhusu wabunge watoro, alisema atahakikisha kuwa kila siku koramu, inatimia bungeni na kwa wale ambao hawatakuwepo ni wenye kazi maalum pekee.

"Kuna kipindi hadi Rais Magufuli, alisema wabunge watoro warudishe posho, mimi kwangu hili litalisimamia vilivyo kuhakikisha kila mtu nashiriki kikamilifu katika vikao vya bunge"alisema

Aidha, alisema katika ofisi za wabunge atafunga mfumo wa mahudhurio kwa njia ya vidole ambapo mbunge atakua anasaini kwanza kabla ya kwenda kufanya kazi za wananchi.

Alisema hali hiyo itasaidia kuondoa tabia ya baadhi ya wabunge ambao wamekuwa hawatekelezi ipasavyo majukumu yao wakati ambao vikao vya bunge jijini Dodoma vinakuwa vimesimama.

Hata hivyo, alisema kuwa katika bunge hilo atahakikisha inakuwepo kamati ya maadili ya bunge yenye meno ambayo haimumunyi maneno ili kuwashughulikia wabunge wanaokwenda kinyume na kanuni za bunge.



Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari Fountain Gate, Japhet Makau, akizungumza na wazazi katika mahafali ya pili ya kidato cha nne, shuleni hapo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Tume umwagiliaji yapewa majukumu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) imeagizwa kuhakikisha inaongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta milioni moja katika miaka mitano ijayo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara katika ofisi ya tume hiyo jijini hapa.

Alisema tume hiyo inapaswa kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 699,715 za sasa hadi hekta milioni moja.

"Ongezeko la eneo hilo lilenge kutanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kufikia asilimia 30 mwaka 2025,"alisema.

Katibu mkuu huyo alisema serikali imejipanga kupitia tume hiyo kuwapo na mabadiliko makubwa ndani yake na kutimiza malengo ikiwamo huduma kuwafikia wakulima ili wanufaike na kilimo cha umwagiliaji. Hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Daudi Kaali, alisema NIRC inatarajia kujenga na kukarabati skimu 384 zitakazogharimu Sh. bilioni 986.8 ili kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Alisema hatua hiyo ni mkakati wa miaka mitano ijayo na zitajengwa kwenye mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Tabora na Katavi na zitaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 400,491.8.

# Mradi boresha lishe wapunguza udumavu

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

UDUMAVU wa watoto katika Wilaya ya Chamwino umepungua baada ya kunufaika na kilimo cha mboga kupitia mradi wa boresha lishe, imeelezwa.

Akizungumza jana na wananchi, Meneja Mradi huo, Jeremiah Mziray, kutoka shirika lisilo la kiserikali la utafiti, ushauri wa kitaalamu na uwezeshaji wa maendeleo ya kiuchumi vijijini (RECODA), alisema mradi huo unafadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya chini ya shirika hilo ambao umewafikia wananchi katika vijiji 39 vya wilaya hiyo.

"Vijiji vyenye idadi kubwa ya watoto waliodumaa ni hivyo 39 na kutokana na ukubwa wa tatizo ndio maana tukapewa jukumu la kuhakikisha tunatoa elimu na kuwafundisha kuzalisha vyakula vya kutosha vyenye virutubisho vingi," alisema.


Alisema hatua hiyo inalenga kupunguza udumavu kwa watoto hasa wenye umri wa miaka mitano. "Mradi ulianzishwa mwaka 2017 kwa ajili ya vijiji 124 vya Mkoa wa Dodoma na Singida ili kupunguza udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kuinua wananchi kiuchumi," alisema. Mkulima Rhoda Mzilani alisema mradi huo licha ya kusaidia kupunguza udumavu lakini pia umefungua fursa ya wao kulima mboga na kuziuza.

"Kwa kweli mboga hizi zimesaidia kwa kiwango kikubwa nimelima nachuma mboga zangu za majani, napika nakula na watoto, hata kuuza nimeuza, kwa kweli mradi huu ni mzuri," alisema.

Naye mkulima Scolastika Machela, alisema fedha ambazo zinapatikana kwa kilimo cha mboga, husaidia kununua mboga aina nyingine ili kuongeza virutubisho.

"Kutokana na kila mtu kulima kulikuwa na tatizo la masoko lakini kwasasa tunashukuru kwasababu kutokana na makao makuu kuja Dodoma, kwa hapa Chamwino Ikulu watu wameongezeka wengi kwa hiyo tatizo la masoko halipo kwa kuwa watu ni wengi,"alisema.

Ofisa Tarafa ya Chilonwa, Mohamed Mfaki, aliwataka maofisa ugani ngazi ya kijiji na kata kuhakikisha wanawatembelea wakulima wote.



## Matukio 57 udhalilishaji yatinga ustawi wa jamii

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

MATUKIO 57 ya udhalilishaji yameripotiwa katika Ofisi ya Ustawi wa Jamii Wilaya ya Wete, Pemba kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Hayo yalisema jana na Ofisa Mipango Wilaya ya Wete, Khadija Mwadini Haji, wakati akiwasilisha ripoti ya matukio ya udhalilishaji katika mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Sheikh Idrisa Abdul-Wakil, Kizimbani, Wete.

Alisema ofisi ya ustawi wa jamii wilaya ya Wete kwa kipindi cha miezi miwili imepokea matukio 57 ya udhalilishaji, 22 yakiwa mvutano wa kimalezi, matano kubaka, matano kulawiti, mawili kutorosha, matatu kunajisi na 20 kutelekeza watoto.

"Kati ya matukio hayo yaliyoripotiwa, tayari matukio 34 yamepatiwa ufumbuzi, sita yanaendelea kusikilizwa katika ofisi hiyo, mawili yamepelekwa katika mahakama ya kadhi na mengine polisi kwa ajili ya upelelezi na mahakamani kwa kusikilizwa.

Alisema kuna vikwazo mbalimbali vinavyowakabili katika kupambana na kesi hizo, ikiwamo kinababa wasio na kazi maalumu kushindwa kutoa huduma kwa watoto waliotelekezwa, na hawajui sehemu ya kwenda kuwakamata.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Siti Suleiman Juma, aliitaka jamii kupaza sauti zao kupinga watoto kushiriki katika shughuli za mikusanyiko, na huwasababishia kufanyiwa udhalilishaji.

"Nimekuwa nikiwaona watoto kwenye harusi, mikutano na mikusanyiko mingine ambayo si mizuri kufika watoto. Tena zaidi utawakuta kuanzia miaka 15 hadi 17 wanazurura na wanaume, jambo ambalo linanitia huzuni," alisema.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Hamad Salim, kutoka Mahakama ya Kadhi Wete alisema kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu, mahakama hiyo ilipokea kesi 19, ambazo talaka za 14, zinazohusu mirathi mbili, kudai huduma moja na mbili ni kutaka idhini.

Mratibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema mbali na kufuatilia taarifa za udhalilishaji, kamati hiyo imetumia muda mwingi kwa ajili ya kutoa elimu ya udhalilishaji kwa jamii, ili kuhakikisha inapata uelewa zaidi kuhusu vitendo hivyo.

"Pia tutumie vyombo vya habari kuelimisha, elimu tumeshatoa lakini bado baadhi ya wanajamii hawana ufahamu juu ya madhara yanayoweza kujitokea iwapo udhalilishaji utafanyika", alisema.

# Kiongozi ataka ushirikiano wa kuijenga Zanzibar mpya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Khamis Mussa, amesema kazi ya kuijenga nchi si jukumu wala kazi ya serikali pekee badala yake kunahitajika ushirikiano wa pamoja na kasi yenye uwajibikaji wa ufanisi.

Khamis alitoa ushauri huo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mwelekeo wa uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, katika suala la uimarishaji wa maendeleo nchini.

Alisema serikali imeanza kubainisha baadhi ya mambo ambayo imedhamiria kuyasimamia katika kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unaendelea kukua na kutoa wigo mpana wa shughuli za kiuchumi na kijamii jambo muhimu ni kudumisha ushirikiano utakaoleta matokeo chanya.

Khamis alisema ili kutimiza hayo, kuna haja kwa watendaji na wananchi wa Zanzibar kuisikiliza kwa umakini mkubwa hotuba itakayotolewa na Rais Dk. Mwinyi ambayo itaeleza dira na mwelekeo wa kiutendaji katika serikali ya awamu ya nane ambayo imedhamiria kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii nchini.

Alisema hatua hiyo itasaidia kutafakari sambamba na kuchambua kwa kina juhudi na mikakati ya serikali iliyokusudiwa katika uimarishaji wa huduma muhimu ambazo zitakuwa ni sehemu ya kuchochea nguvu mpya ya uchumi wa Zanzibar.

"Ni vyema watu wote kuhakikisha tunafatilia kwa karibu hutuba ya Dk. Mwinyi ambayo anatarajia kutoa muelekeo wote wa uchumi na mwenendo mzima wa uwajibikaji wakati akizindua baraza la Wawakilishi Novemba mwaka huu," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, aliwataka wananchi wajitayarishe kupokea kasi ya maendeleo na wawe tayari kushiriki katika mipango ya ujenzi wa maendeleo kwa kufanya kazi kwa bidii na kuacha mazoea.

"Tuondokane na utamaduni wa ufanyaji wa kazi kwa mazoea badala yake kila mmoja awajibike ipasavyo kwa lengo la kuijenga Zanzibar mpya ya maendeleo endelevu katika sekta mbali mbali," alisema.

Ayoub alitumia nafasi hiyo kutoa rai kwa wananchi wa mkoa huo kufuatilia kwa karibu hutuba itakayotolewa na Dk. Mwinyi kupitia vyombo vya habari ambayo inategemewa itabeba dira na mikakati ya maendeleo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Pia aliwataka watendaji mara baada ya kuisikiliza kwa makini na kutafakari ni wajibu kuiunga mkono na kuisimamia vyema ili malengo yatimie kwa wakati sahihi uliokusudiwa.

Alihimiza umuhimu wa watu kubadilika kimawazo huku wakiweka matarajio makubwa ya kiuchumi kwa kufanya kazi kwa bidii sambamba na kutumia fikra na mipango endelevu itakayosaidia kuweka kipaumbele cha kujali na kuthamini uzalendo wao.



Mkufunzi Sanje Lufwelo (wa pili kushoto), akitoa elimu kwa wajasiriamali kuhusu matumizi ya vifungashio ili kuboresha bidhaa zao, katika mafunzo yaliandaliwa na chama cha waandishi wa habari wanawake Tanzania (TAMWA), upande wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Salamu zamiminika kumpongeza Dk. Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SALAMU za pongezi zimendelea kutolewa na viongozi mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kutokana na ushindi wa urais wa Zanzibar alioupata Rais Dk. Hussein Mwinyi katika uchaguzi mkuu uliofanyika hivi karibuni.

Salamu za pongezi za hivi karibuni zimetolewa na Mtawala wa Ras Al Khaimah, Sheikh Saud bin Saqr Al- Qasimi. Katika salamu hizo, Sheikh Saud bin Saqr Al-Qasimi alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa ushindi huo mkubwa alioupata katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Ushindi huo mkubwa, Sheikh Saud bin Saqr Al-Qasimi alieleza kuwa ni wa mafanikio makubwa yanayotokana na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Sheikh A-Qasimi alimwahidi Rais Dk. Mwinyi kwamba Ras Al Khaimah itaendeleza uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kwa manufaa ya pande zote mbili.

Naye Rais Mwinyi kwa upande wake, alitoa shukurani zake za dhati baada ya kupokea salamu hizo kutoka kwa kiongozi huyo wa Ras Al Khaimah na kueleza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi wake inazisamini na itaendeleza uhusiano na ushirikiano uliopo.

Wakati huo huo, Dk. Mwinyi alimpongeza kiongozi wa Oman, Sultan Haitham Bin Tariq Al Said pamoja na wananchi wake kwa kusherehekea siku ya uhuru wa taifa hilo.

Katika salamu hizo Dk. Mwinyi alimhakikishia kiongozi huyo wa Oman kuwa Zanzibar itaendeleza uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo sambamba na kuimarisha udugu uliopo kati ya wananchi wa Oman na Zanzibar.

Sambamba na hayo, salamu hizo zilieleza kuwa siku hii adhimu inaendelea kutoa nafasi zaidi ya mashirikiano kati ya pande mbili hizo pamoja na kupongeza juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Oman katika kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha sekta mbali mbali za maendeleo.

Rais Mwinyi alimtakia heri, mafanikio, afya njema na maisha marefu kiongozi huyo wa Oman pamoja na wananchi wake wote sambamba na kukuza na kudumisha amani na maendeleo yaliopatikana nchini humo.

Oman ilipata uhuru wake kutoka ukoloni wa Kireno Novemba 18, 1660 chini ya kiongozi na mwasisi wa taifa hilo, Iman Sultan Bin Saif Bin Malik Al Yarubi, ambaye alisimamia kung'oka kwa koloni hilo kutoka nchini Oman pamoja na bandari zote za nchi hiyo zilizokuwa chini ya utawala wa Kireno.



LINAH
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI NOVEMBA 7, 2020



## WAMERUDIANA

# Diamond, Zari presha inapanda

MWANAMUZIKI maarufu nchini Diamond Platnumz na mama watoto wake Zari, wameanza kufungua ukurasa mpya baada ya kupigana kibuti na kisha kuwa mbali kwa zaidi ya miaka miwili.

Ujio wa Zari hapa nchini akiwa na watoto wake wawili, ni ishara nzuri kuwa wawili hao wameamua kuweka tofauti zao pembeni ili kuandaa barabara mpya ya uhusiano wa kimapenzi.

Hata hivyo, Zari mwenyewe akizungumza mara baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, alionyesha kila dalili kwamba wao sasa ni wamoja.

"Hakuna shida kuja hapa Tanzania nyumbani kwa watoto wangu, wapo wanaouliza nitalala wapi kwa kipindi hiki, jibu hapa naweza kuwa hotelini au nyumbani, kote nitakuwa na furaha," alisema.

Kwa kauli yake hiyo ni dhahiri kwamba yeye na watoto wake watafikia nyumbani kwa Diamond na huko ndipo watu watashuhudia penzi jipya likichanua baina yao.

Hata walipokuwa uwanjani hapo, Diamond na Zari hawakuonyesha kama wao ni wazazi, bali walidhihirisha wao ni wapenzi kutokana na kufanyiana matendo ya kimahaba kama vile kupigana mabusu na kukumbatiana.

Kama wawili hao wameamua kurudiana na kuanza ukurasa mya, Je, penzi lao litajibu matakwa ya mashabiki wao ambao wanataka kuwaona wakiwa Pamoja? Yote hayo yanahitaji muda ili kupata jibu.

BASI SAWA

## Kumbe Zee Cute anafaa kuwa bondia

MWANAMUZIKI Zee Cuty, amesema ngumi zilizozuka kati yake na msanii mwenzake wa kike, Gigy Money, ulitokea kwa bahati mbaya.




Akizungumza na EATV, Zee Cute, amesema kwenye ugovi huo yeye alikuwa na akili timamu, lakini hafahamu kama Gigy, alikuwa katika hali gani.

"Sina tofauti na mtu yeyote kama ilitokea ilikuwa ni kwa bahati mbaya tu, mimi nilikuwa na akili timamu labda mwenzangu sijui alikuwa na akili gani, situmii kilevi,sielewi wala sidangi hata ngumi zenyewe siwezi, hatukupigana na mimi sio bondia ila tulipishana kauli sijajua chanzo ni nini

## Amber Lulu hujui binadamu kazi?

MWIMBAJI nyota wa BongoFleva, Amber Lulu, amekana kuwa na ujauzito wa Uchebe, akisema watu wanapenda kumzulia maneno mabaya.

Amesema maisha yake yanabaki kuwa ni siri na kamwe hawezi kuyaweka hadharani kama baadhi ya watu wanavyotaka, na yote yanayosemwa ni husda juu yake.

"Maisha yangu siyaweki sana hadharani, mimi ni mtu wa siri sana, hata kwa watu waliowahi kuwa karibu na mimi wanajua hilo, kwa hiyo usiri wangu unawatesa na ndiyo maana wanahangaika wananipa vitu kibao mara naambiwa nina mimba ya Uchebe lakini sio kweli" ameeleza Amber Lulu





## Linah ukiboronga hapo watakucheka

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Linah Sanga, ameshauriwa kutulia na mpenzi wake mpya, ambaye amemuweka hadharani hivi karibuni.

Baadhi ya mashabiki ambao walishiriki picha aliyoweka katika ukurasa wake wa Istagram ambayo ilimuonyesha akiwa na mpenzi wake huyo, mashabiki hao walimpongeza na kueleza ni hatua nzuri kwake.

Hata hivyo katika ujumbe wake, Linah alisema ameamua kumuweka hadharani baada ya baadhi ya watu kumsema vibaya kwamba hakai na wanaume, hivyo ameamua kuwaonyesha Watanzania kwamba anaweza kudumu na mwanamume.



## Msimchukulie poa Chid Benzi

RAPA Mkongwe, Chid Benzi, amesema kuna baadhi ya wanamuziki walikuwa wanamchukulia poa, lakini baada ya kuwakazia kisanii sasa wameanza kumkubali.

Akizungumza hivi karibuni, Chid Benzi, ameeleza kwamba huko nyuma alikuwa mkorofi kiasi ambacho alijenga maadui wengi na baadhi wakimuona kama ni mgeni katika jiji la Dar es Salaam.

"Zamani nilikuwa mkorofi sana mpaka baadhi ya wanamuziki waliniona naleta ushamba kutoka kijijini, lakini ukweli nimezaliwa Ilala na ninajua kila kitu kuhusu jiji hili. Wale waliodhania mimi mshamba leo wamekubali wenyewe kwa jinsi ninavyoishi," amesema.

## UKIKUTANA NA HAWA SALI SALA ZA MWISHO

**Na Adam Fungamwango**

KWA wale waliokuwa wakipenda kuangaliza filamu za zamani za kibabe, ziwe za kizungu au kihindi, watakuwa wanakumbuka mambo mengi.

Kabla ya huko mbele ya safari kuangalia masteringi wa filamu mbalimbali za kizungu na kihindi waliovuma na kutikisa anga la mapicha ya kizamani, leo tutawaangazia waigizaji waliokuwa wakiziweka roho za watazamaji juu, kuanzia mwanzo hadi mwisho wa picha hizo.

Hawa ni wale waigizaji waliokuwa wakiigiza kama maadui kwenye filamu hizo.

Walizifanya kazi zao vizuri zaidi kiasi cha hata waliokuwa wanaangalia filamu kudhani kuwa hata maisha yao halisi ndiyo walivyo.

Leo tutawaangalia waliokuwa wakicheza kama maadui kwenye picha cha kihindi enzi hizo.

**Amrish Puri 'Mzee Ashanti'**

Ndiye muigizaji katili zaidi kwenye filamu nyingi za kihindi. Ndiye muigizaji adui anayejulikana, kupendwa na kuchukiwa sana na Wabongo waliokuwa wakiangalia filamu za kihindi wakati huo miaka ya '80 hadi mwanzoni mwa '90.

Watoto na vijana wa Kibongo walimpachika jina la Mzee Ashanti, kiasi cha wengi kutojua hata jina lake halisi. Wengine walimwita 'Mugambo' au 'Adui Kubwa'. Wenyewe wanakwambia picha la kihindi bila Mzee Ashanti kuwa adui halinogi.

Anatajwa kuwa ndiye muigizaji katili zaidi kupata kutokea kwenye filamu za kihindi.

Ni mwigizaji aliyejipatia sifa kubwa duniani kutokana na kuigiza kiuhalisia jinsi katili halisi anavyopaswa awe. Na ndiyo maana amekuwa ni mmoja wa waigizaji waliopata tenda ya kuigiza filamu nyingi sana za kihindi wakati huo na nafasi yake ikiwa ni hiyo hiyo ya adui mkuu.

Alifariki mwaka 2005 na kuacha jina kubwa si nchini India tu, bali duniani kote ikiwemo Bongo.

**Danny Denzongpa**

Wabongo wanamwita Deni Zompa. Ni mwigizaji mhindi mwenye asili ya Nepal, ambaye naye amejikita zaidi kucheza nafasi ya adui.

Ukiacha mzee Ashanti, Deni ni mmoja wa waigizaji katili zaidi kwenye filamu za kihindi, akiwa na uwezo mkubwa wa kuutumia mwili wake kwenye sanaa za mapigano, achilia mbali, silaha mbalimbali.

Watoto wa kibongo wakati huo walikuwa wanasema bora ukutane na simba kuliko kuingia kwenye anga za Deni.

**Ranjeet**

Huwezi kuwataja maadui kwenye filamu za kihindi bila kumtaja mmoja wa watu waliokuwa wakizifanya zisisimue zaidi wakati huo, aitwaye Ranjeet. Watoto na vijana wakati huo wao walikuwa wakimwita 'Lanjiti'.

Ni mwigizaji katili mwenye roho mbaya, ambaye naye alikuwa wakiwaweka roho juu mashabiki wa filamu hizo.

**Rajesh Khanna**

Ni mmoja wa waigizaji wazuri akicheza kama adui kwenye filamu mbalimbali za kihindi. Pamoja na filamu mbalimbali, lakini unyama wake waliufanya kwenye filamu ya 'Disco Dance' ya Mithun Chakraborty.

**Shakti Kapoor**

Ni mmoja wa waigizaji maarufu wa muda mrefu nchini India ambaye naye huigiza kwenye sehemu za ubabe ubabe, na pia amekuwa akilitendea haki eneo hilo analopangwa kucheza.



## Mfuko Mweusi: Siri inapopenya mitaani

**Na Adam Fungamwango**

MARA nyingi binadamu hupata matatizo kwenye maisha yake akiamini ni siri, lakini anajikuta yote yanasambaa mitaani bila kujua nani kavujisha.

Siku zote siri za mtu hutolewa na mtu aliye karibu naye.

Ndiyo maana watu wa intelijensia wana msemo wao wa 'usimwamini mtu yoyote hata kama ni maiti.' Maiti huwa haizungumzi na wala haijui lolote lile linalotendeka duniani. Lakini badi unaambiwa kuwa usiiamini. Hii ni kukupa msisitizo kuwa hutakiwi kuamini kitu chochote au mtu yeyote kwa siri au mambo ambayo yanatakiwa yawe siri yako.

Filamu ya 'Mfuko Mweusi' ina mtazamo huo, unaowataka watu kuwa makini, kwani unaweza kumwamini mtu, lakini akawa si mtu mzuri.

Inaanzia kwa Bi Staa. Huyu ni mwanamke shugamami. Anampenda kijana mmoja kibenteni.

Binti ya Bi Staa aitwaye Merina anachukia kuona mama yake anatembea na kijana mdogo, lakini anapakiwa maneno ya mama yake.

Mwisho wa siku yalipozidi akafukuzwa




nyumbani ili mama apate nafasi ya kutanua vizuri na kibenteni chake.

Merina anakwenda kuomba kazi kwenye baa. Huko nako kama kawaida anakutana na changamoto kibao.

Huku alikokuacha nako, mama yake akaanza kugombana na kibenteni wake hadi akamtimua.

Kibenteni akanyang'anywa khanga mchana kweupe, ng'ombe anakula majani.

Kwa bahati mbaya sana, Merina akaingia kwenye mapenzi ya mtu mmoja anaitwa Kupa.

Huyu jamaa si mtu mzuri. Ni jambazi, tena mdhulumati. Merina hajui. Kutokana na kuhangaika, akahamia kabisa kwa mpenzi wake huyo.

Kupa akiwa ofisini anapanga mipango ya kwenda kuiba kifuko cheusi. kwa sasa yeye ni mkubwa, anatuma vijana wake kwenda kuifanya kazi hiyo.

Hata hivyo, baada ya kuupata anafanya mpango wa kuwadhulumu wenzake. Hata hivyo mpenzi wake Merina hajui hilo. Siku hiyo anakuja kutekwa na majambazi ili akawaonyeshe alipo mpenzi wake. Kupa anapatikana na Merina akaachiwa.

Hata hivyo, jambazi wa kike papo hapo anataka kumgeuka mwenzake baada ya kuupata mfuko mweusi unaoonekana kuwa una pesa au mali yenye thamani.

Hiyo inampa fursa jambazi aliyekuja naye kumchapa risasi demu yule. Lakini hilo linakuwa limempunguzia kazi Kupa, alimmalizia aliyebakia.

Alichukua mfuko mweusi, akaenda kumkabidhi mpenzi wake Merina. Akamwambia aondoke eneo lile kwani limekuwa ni la hatari. Alipotokomea, aliwasiri jambazi mwingine naye akiutaka mfuko huo weusi. Ngumi zikafumuka, Kupa akamalizia na kutoa bastola akampiga jambazi mwezake, lakini ghafla na yeye akatwangwa risasi ya kichwa.

Ilikuwa ni kazi ya askari polisi ambaye alijitokeza na kuanza kupigia simu wenzake waje wachukue miili ya majambazi waliokufa kwenye mapambano. Kifuko au mfuko mweusi ukawa mikononi mwa Merina aliyerejea kwa mama yake akiwa amenona.



# Lil Wayne kaachwa na mrembo kiaina

RAPA mkongwe wa Marekani, Lil Wayne, amekimbiwa na mpenzi wake baada ya kutangaza anamuunga mkono Rais Donald Trump.

Mwanamuziki huyo staa, ameachwa na mrembo huyo Denise Bidot, kupitia Istagram baada ya mwanamke huyo kuandika kwamba " Wakati mwingine mapenzi yanafika mwisho," huku akiweka emoji ya moyo ikiwa umevunjika katikati.

Kulingana na mtandao wa PageSix, Denise ameamua kuachana na Wayne, baada ya kutangaza wamefanya makubaliano na kiongozi huyo jinsi ya kuwasaidia Waafrika.



## Mercy hata pilau hukuliandaa?

MSHINDI wa shindano la Big Brother Nigeria, Mercy Eke, ametangaza rasmi kuwa yupo kwenye ndoa na kwamba mambo ya zamani kwake yamekuwa kama mapito.

Akiandika katika ukurasa wake wa Istagram, Mercy, amesema ndoa yake na mwanamume ambaye hakumtaja imefungwa miezi mitatu iliyopita, lakini hakutaka kuiweka wazi.

Amesema penzi lake na Ike limekwisha siku nyingi na sasa anaendelea na maisha yake na mume wake wa sasa.

## Card B kweli wewe nataka sitaki

MWANAMUZIKI wa kike wa Hip hop kutoka Marekani,Cardi B, ameendelea kuwashangaza mashabiki wake baada ya kwenda mahakamani kuomba talaka kwa mume wake Offset.

Kulingana na mtandao wa PageSix, rapa huyo aliwasilisha ombi la talaka siku ya Jumatatu, Novemba 2, mwaka huu.

Hata hivyo wanandoa hao kila mara wanatangaza kuachana na kisha kurudiana tena, jambo ambalo linawachukiza mashabiki wao.

Hata hivyo, jaji anayesikiliza kesi hiyo, bado hajasaini ombi hilo.





## Beyonce aikumbuka 'Black is King'

MWIMBAJI na mtunzi wa nyimbo wa Marekani, Beyoncé. Amesema mwaka 2020 umekuwa muhimu kwake baada ya kutoa albamu ya "Black is King" ambayo iliunganisha vipaji kutoka Afrika.

Akihojiwa na jarida maarufu la Vogue, Beyoncé, alifichua kuwa upangaji wa albamu yake ilianza katika mazingira ya nyumba yake, kisha alisafiri hadi Afrika kuchukua picha zaidi.

"Kazi ilianza rahisi, katika ua wa nyumba yangu, kisha nilitaka kufanya video moja au mbili za albamu ya The Gift, basi ilikua kama masihara hivi, lakini nilikwenda Nigeria, Ghana, Uongereza, Los Angeles, Johannesburg, na KwaZulu-Natal, Afrika Kusini," amesema.

## Uchemba usiishie uchumba tu

MWIGIZAJI maarufu wa filamu za watoto kutoka Nollywood, Williams Uchemba, amemchumbia mpenzi wake wa muda mrefu, Brunella Oscar.

Staa huyo alitoa taarifa kupitia ukurasa wake wa Istagram, akisema kuna wakati kila mwanamume anahitaji kuwa karibu na mwanamke anayempenda.

"Hoja yangu kuu ni kumshukuru Mungu kunipa mwenzi wangu wa  maisha ambaye anaweza kuelewa," ameandika Uchemba.



MAKALA

# JIMBO LA TIGRAY

## ■Uvumilivu wamshinda Abiy Ahmed
## ■Kiburi chao kuibua vita kamili?



Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed. **PICHA : MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

NI dhahiri vita kamili ya wenyewe kwa wenyewe inainyemelea Ethiopia, baada ya serikali ya jimbo la Tigray, kuasi na kudai kujiondoa kutoka serikali kuu.

Mashambulio ya kijeshi yanaendelea katika jimbo hilo liloko kaskazini mwa nchi hiyo na kuzusha hofu kwa wananchi wa eneo hilo.

Mgogoro huo ulianza baada ya utawala jimbo hilo unaongozwa na chama cha TPLF, ambacho kiliongoza nchi hiyo kwa miongo kadhaa, kuahirisha uchaguzi wa eneo hilo kutokana na kuhofia kusambaa kwa virusi vya Corona.

Waziri mkuu Abiy Ahmed, aliagiza jeshi la nchi hiyo kushambulia eneo la Tigray , kufuatia tukio la wanamgambo hao kushambulia kambi moja ya kijeshi na kusababisha vifo vya askari na wengine kujeruhiwa.

**HALI YA WASIWASI**

Chama cha TPLF kimekuwa kikikosana na serikali ya Abiy tangu alipochukua madaraka 2018.

Waziri Mkuu huyo ambaye anaonekana kama kiongozi anayetaka kuleta mabadiliko, alipoingia madarakani aliwashutumu maofisa wa serikali zilizopita kwa kukumbatia ufisadi na ukiukaji wa haki za binadamu, na wengi wa maofisa wakuu wa chama cha TPLF waliondolewa serikali kuu.

Mkuu wa ujasusi wa Ethiopia, aliapa kuendelea na operesheni ya kijeshi katika jimbo hilo, licha ya kutolewa wito wa kimataifa wa kutaka mamlaka nchini humo kusitisha operesheni hiyo.

Mzozo kati ya chama cha TPLF, ambacho wakati mmoja kilikuwa mshirika ndani ya muungano serikali ya Ethiopia, na Waziri Mkuu Abiy Ahmed, umekuwa ukitokota kwa miezi kadhaa, na ulikuja kujitokeza wazi baada ya jimbo hilo kukaidi amri ya serikali kuu na Tume ya uchaguzi na kufanya uchaguzi.

Waziri mkuu alitoa amri kwa jeshi kushambulia Tigray, baada ya kueleza shambulio hilo linabidi lifanyike kwa kuwa walisababisha vifo vya watu wengi wasio na hatia.

**CHANZO CHA MVUTANO**

Uchaguzi wa Septemba huko Tigray, ambao serikali ya shirikisho ilikuwa imeahirisha nchi nzima kwa sababu ya janga la corona, inachukuliwa kuwa ndio sababu ya kuzorota kwa uhusiano wao.

Hata hivyo, mivutano imekuwa ikijitokeza mara kwa mara kati ya serikali kuu na TPLF, muda mfupi baada ya Abey kuingia madarakani mnamo 2018.

Baada ya Abiy kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu, aliwashutumu maofisa katika serikali zilizopita kuwa mafisadi, wakiukwaji wa haki za binadamu na kibaya zaidi aliondoa takwimu muhimu za TPLF ndani ya serikali kuu.

Hatua hiyo, ilimkumba mkuu wa zamani wa ujasusi na ofisa mwandamizi wa TPLF, Getachew Asefa, ambaye alitaka kukamatwa, lakini alikimbilia Tigray, ambako bado anaishi kama mkimbizi.

Aidha, Abiy mwaka jana alijumuisha vyama vyenye misingi ya kikabila ambavyo viliunda umoja wa EPRDF ambao ulianzisha chama cha PP.

Hatua hiyo ilipingwa vikali na TPLF, ikieleza inaweza kuleta mgawanyiko ndani ya nchi hiyo.

Mapema mwaka huu, mpasuko huo uliongezeka zaidi baada ya serikali ya shirikisho kuhairisha uchaguzi wa kitaifa.

Uamuzi wa Tigray wa kutaka kupiga kura yake mwezi Septemba, ilikuwa kitendo sawa na uasi dhidi ya serikali ya shirikisho. Bunge la shirikisho lilitaja mchakato huo kuwa ni haramu.

TPLF hapo awali ilikuwa imetoa vitisho vya kujitenga, ikinukuu kifungu katika katiba ya shirikisho ambacho inaruhusu haki ya kujitawala, pamoja na haki ya kujitenga.

"Hatutawahi kurudi nyuma kwa mtu yeyote ambaye ana nia ya kukandamiza haki yetu iliyoshindwa kwa bidii ya kujitawala na kujitawala," anasema kiongozi wa mkoa huo, Debretsion Gebremichael.

Ilipofikia mwezi wa Oktoba, serikali ya shirikisho iliamua kukata uhusiano na mkoa wa Tigray huku bunge likapiga kura kusitisha msaada wa bajeti kwa jimbo jilo.

**TPLF KILITOKA WAPI?**

Tangu kupinduliwa kwa Waziri Mkuu wa zamani, Mengistu Haile Mariam, mwaka 1991 na kufikia 2018, TPLF ilikuwa mshirika mkuu katika uongozi wa taifa hilo, na vile vile kuendesha jimbo hilo.

TPLF ilihusika moja kwa moja na kifo cha Mengistu, na baada hapo ilitawala siasa na uchumi wa taifa hilo.

Viongozi wengi akiwamo Debretsion, walikuwa maofisa wa ngazi za juu katika serikali kuu kwa muda mrefu.

Utawala wa Tigray unaona mageuzi yanaoyofanywa na Abiy ndani ya serikali ya shirikisho kama jaribio la kujijenga na kuharibu mpangilio wa sasa wa shirikisho.

Pia chama hicho kinachukia uhusiano wa kidiplomasia ulioanzishwa na waziri huyo mkuu na Rais wa Eritrea, Isaias Afwerki.

Abiy alishinda Tuzo ya Amani ya Nobel mnamo 2019 kwa juhudi zake za kuleta amani na adui wake wa muda mrefu na Eritrea.

Lakini TPLF inahisi makubaliano hayo yanaondoa masilahi ya Tigray na inataka kupata uhakikisho zaidi kuhusu kuhusu makubaliano hayo. Kwa upande wake, Abiy, anaamini maofisa wa TPLF wana njama ya kutaka kudhoofisha mamlaka yake.

**ERITREA INAHUSIKA?**

Mgogoro wa mpaka kati ya TPLF na serikali ya Eritrea, umedumu kwa muda mrefu na kusababisha kuibuka kwa vita kati ya Ethiopia na Eritrea mwaka 1998 hadi 2000.

Mabishano yalitokana kuhusu eneo karibu na mji wa Badme, ambao Tigray inadai ni miliki yake, huku

Eritrea inataka kutii amri ya tume ya mpaka inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa, ambayo inaipa mamlaka nchi hiyo kuutawala.

**JE VITA KAMILI ITAIBUKA?**

Kiongozi wa mkoa wa Tigray, anasisitiza wako tayari kupigana kwa kutetea eneo hilo, na kueleza eneo hilo sawa na eneo la kufa au kupona.

Anawataka Watigray kuelewa hali hiyo na kufanya maandalizi muhimu kwani lolote linaweza kutokea. "Tumeandaa jeshi letu, wanamgambo wetu na kikosi chetu maalum. Maandalizi yetu yanalenga kuzuia vita, lakini ikiwa tunataka kupigana, tuko tayari kushinda," anasema Debretsion.

Ofisi ya Waziri Mkuu imeishutumu TPLF kwa kuendelea na vitendo vya uchochezi na vurugu ambavyo vimevuka mipaka.

Kuna hatari mzozo wa Tigray, kama haujasuluhishwa haraka unaweza kulipuka kuwa vita kamili na kuleta hali ya wasiwasi nchini humo.

**KWA MSAADA WA BBC**

# CWT iliposhikana mikono na mmiliki wa shule za umma kukubali mageuzi

■Mabilioni ya shilingi; majengo hadi darasani
■Mitihani; kazi za mikono hadi kompyuta
■Walimu wapiga makofi 'madai yetu poa'

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), hivi karibuni kiliadhimisha Siku ya Walimu Duniani, kwa kufanya kongamano la kutathmini mafanikio na changamoto zinazowakabili walimu nchini.

Shuguli hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa LAPF jijini Dodoma hapa, ilihudhuriwa na walimu kutoka pande mbalimbali hapa nchini, mgeni rasmi akiwa Jenister Mhagama, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,

Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, altumia fursa hiyo kukiri kufunguliwa milango ya kutatuliwa matatizo katika sekta ya elimu nchini, baadhi ya mambo yaliyokuwa kikwazo katika siku zilizopita.

Seif anataja vikwazo vilivyowakabili ni malimbikizo ya mishahara na madai yao mbalimbali, ambayo serikali ilishaanza kuwalipa madeni na madai sugu yaliyokuwapo.

Aidha, Seif anasema walimu wataendelea kuishukuru serikali katika hatua ya kuanza kupandisha madaraja ya walimu kazini kwa waliostahili kufanyiwa hivyo, pamoja na kuwekewa mazingira bora ya kazi.

"Kwa kweli sisi walimu tutaendelea kuishukuru serikali, imetatua changamoto zetu nyingi ambazo zilikuwa zikitusumbua, pia mazingira mazuri ya kazi yamewekwa ikiwamo nyumba za kisasa za walimu kujengwa", anasema Seif.

**MABORESHO YALIVYO**

Katibu Mkuu huyo, anaorodhesha hatua mbalimbali serikali ilichukua kuhakikisha inatoa elimu bora kwa watoto wa Kitanzania, ikiwamo kutolewa elimu bila ya malipo ngazi ya chini kielimu, hadi kidato cha nne katika shule za serikali.

Pia, anataja hatua zinazomfanya mwalimu afanye kazi katika mazingira mazuri na kumhamasisha kutoa elimu bora kwa wanafunzi wake, ambao ndiyo watarajiwa wa kujiunga na elimu ngazi ya juu, vikiwamo vyuo vikuu.

Kwa mujibu wa katibu mkuu huyo, serikali imefanya ukarabati mkubwa kwenye shule kongwe 89 nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 84, ukihusisha maboresho ya miundombinu ya barabara, kuajiri wasanifu wa maabara 297, hali inayomsaidia mwalimu kutoa elimu bora ndani ya uchumi wa kisasa.

Vilevile, maboresho hayo ya mahitaji ya taaluma, yamefanyika kwa ujenzi wa shule mpya za msingi 905 na sekondari 228, hadi kufikia Juni mwaka huu.

**WALIMU WA SAYANSI**

Katika kuongeza tija ndani ya taaluma na dunia ya kisasa, inaelezwa serikali iliongeza walimu wa masomo ya sayansi na hisabati katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Ni hatua iliyoendana na kuajiri jumla ya walimu 7,218 na kati yao 5,528 walikuwa wa masomo ya sayansi na hisabati sawa na asilimia 79.35.

Pia, kutokana na mabadiliko katika mfumo wa uendeshaji uchumi wa kisasa, mwalimu amwekwa sawa kuendana na mahitaji ya kitaaluma kuhakikisha yanayofundishwa shuleni yanaendana na mahitaji ya uchumi na maendeleo ya Taifa.

CWT inaeleza kuwa serikali kupitia Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - TAMISEMI), kuna jumla ya walimu 70,717 waliojengewa uwezo wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kupitia programu mbalimbali za kisasa katika kompyuta.

**SURA YA MAGEUZI**

Hadi sasa, serikali katika kukuza na kuendeleza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu, imeongeza nafasi za elimu ya juu na taasisi za tafiti katika maendeleo ya sayansi na kuwezesha matumizi ya mbinu za kisayansi katika maendeleo ya ya kisasa katika sekta ya uchumi, ikiwamo viwanda na kilimo.

Elimu bora inatarajiwa kuchochewa ubunifu na tija katika uzalishaji, ambao unachochea ubunifu katika sekta ya Kilimo, Viwanda, Uvuvi, Madini na Nishati.

Kongamano hilo lilifahamishwa kuwa, elimu ya shule sekondari, vyuo vya elimu ya juu na ufundi stadi, vina mchango mkubwa katika ukuzaji uchumi wa nchi, hata serikali ikaamua kuanzisha vituo vinne vya umahiri katika Teknolijia ya Habari na Mawasiliano ya Umma (TEHAMA).

Vyuo hivyo vinatajwa kuwa ni vnayofundisha masuala ya usafiri wa anga, nishati jadidifu na mazao ya ngozi, vyote vikitolewa katika vyuo anavyovitaja;Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na Chuo cha Usafirishaji Arusha, kupitia mradi unaoatajwa kwa jina, East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP).

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (BMT) Dk. Charles Msonde, alielezea maboresho ya utoaji elimu ya msingi na sekondari nchini kwa maendeleo ya Taifa.

Dk. Msonde, anataja yaliyofanywa na serikali katika kuboresha utendaji kazi wa walimu nchini, ni pamoja na kutambua umuhimu wa Ofisa Mitihani katika maendeleo ya nchi.

Anasema maboresho makubwa ya kiutendaji kwa walimu yamefanyika, lengo ni kuhitimisha utoaji elimu bora, akirejea walikotoka kabla ya mwaka 2015, kwamba usajili wa watahiniwa shuleni ulifanywa na walimu wakuu au wakuu wa shule na maofisa elimu, waliosajili kwa mkono.

Katibu huyo mkongwe aliyedumu katika baraza hilo kwa muda mrefu, anaeleza kwamba baadaye taarifa hizo ziliwekwa kwenye nyenzo za 'CD' wahusika walizosafiri nazo kukabidhi katika ofisi za Baraza la Mitihani.

Anaeleza mageuzi yaliyopo sasa, ni kwa serikali kuamua kuwajengea uwezo na mazingira mazuri walimu, kwa kuunda mfumo wa usajili kidigitali, mradi uliogharimu Sh. billioni 2.7.

Dk. Msonde anajivuna kwamba serikali imwemuwezesha ofisa mitihani kwa kumpa miundombinu ya kuchapa na kufunga mitihani, pamoja na nyaraka zake kwa kutumia mashine zilizogharimu Sh. bilioni 10.013.



Rais wa CWT, Leah Ulaya, alipozungumza na walimu katika kongamano linalofanyika kila mwaka.
**PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU.**



Walimu wakiwa katika mkutano wao jijini Dodoma, hivi karibuni.

## HABARI KIMATAIFA

# UN yatia hofu mapigano Tigray

**ADIS ABABA, Ethiopia**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Gutteres, ameelezea wasiwasi wake kuhusu mapigano yanayoendelea katika jimbo la kaskazini mwa Ethiopia la Tigray.

Wanajeshi wa serikali kuu wanapambana na kundi lenye nguvu la kikabila ambalo liliuongoza utawala wa jimbo hilo kwa miongo mingi.

Guterres, alisema utulivu wa Ethiopia ni muhimu kwa eneo zima la Pembe ya Afrika.

Alitoa wito wa kusitishwa kwa mapigano hayo na kutafutwa suluhisho la mgogoro huo kwa njia ya amani.

Mfanyakazi mmoja wa kiutu aliliambia shirika la habari la Reuters kuwa milio ya hapa na pale ya makombora yalisikika jana asubuhi karibu na mpaka wa Tigray na Amhara.

Serikali ya Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, imewakusanya wanajeshi kutoka zehemu zote nchini humo na kuwapeleka Tigray, baada ya siku mbili za mapigano kati ya askari wa serikali na Jeshi la Ukombozi wa Watu wa Tigray ( TPLF).

**DW**

## Marekani, Uingereza zahusishwa miradi ya ulinzi

**BRUSSELS, Ubeligiji**

UMOJA wa Ulaya (EU) umepitisha kanuni mpya ambazo zitayaruhusu mataifa yasiyo wanachama wa umoja huo, Marekani au Uingereza kushiriki katika miradi ya usalama.

Hadi sasa miradi 47 imeanzishwa chini ya usimamizi wa Umoja huo, kupitia mpango wa ushirikiano wa muundo wa kudumu, ambao kwa ufupi unaitwa (PESCO).

Utekelezaji wake unaanzia katika kujenzi wa vituo vya nguvu za kijeshi na kuboresha ndege za kivita na vifaru.

Kila mradi unaratibiwa na kundi dogo miongoni mwa nchi wanachama.

**DW**




Joe Biden, anaelekea kushinda dhidi ya Rais Donald Trump. **(PICHA: THE NEW YORK TIMES)**

# Polisi yawachunguza watuhumiwa ugaidi

**VIENNA, Austria**

KIKOSI cha Polisi nchini Ujerumani, kimevamia maeneo la makazi na maduka ya watu wanne wanaohusishwa na mshukiwa aliyehusika shambulizi moja la kigaini nchini Austria.

Mshukiwa huyo inadaiwa anaunga mkono kundi moja linalojiita Dola la Kiislamu, (IS) alifanya shambulizi katika mji wa Vienna, wiki hii.

Idara ya polisi ilisema maofisa wake wakiwamo wa kikosi cha kupambana na ugaidi, walipekua makazi katika maeneo ya Osnabrueck, Kassel na Pinneberg.

Polisi ilisema licha ya watu hao kufanyiwa upekuzi, kwa sasa hawashukiwi katika tukio hilo lilotokea siku ya Jumatatu ambalo lilikuwa la ufyatuaji risasi.

Ushahidi unaonyesha kuwa wana uhusiano na mshambuliaji huyo. Serikali ya Austria ilimtambua mshambuliaji huyo kuwa ni Kujtim Fejzulai, (20), raia wa nchi mbili za Austria na Macedonia Kaskazini,

Awali mtuhumiwa huyo alihukumiwa kwa kujaribu kujiunga na IS nchini Syria na aliachiliwa huru mapema mwezi wa Desemba mwaka jana.

**DW**

# Wabunge Libya wazungumzia amani

**RABAT, Morocco**

WABUNGE wa serikali ya Libya na upinzani wanaotawala eneo kubwa la mashariki ya nchi hiyo, wamekutana kwa mazungumzo ya amani nchini Morocco.

Wanasiasa hao walikutana juzi katika mji wa pwani wa Bouznika, kusini mwa mji mkuu wa Rabat, wakizungumzia mpango wa amani kabla ya mkutano mkuu utakaofanyika Novemba 9 mwaka huu nchini Tunisia.

Mazungumzo hayo yalitokana na makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyosimamiwa na Umoja wa Mataifa na kutiwa saini nchini Uswisi mwezi uliopita.

Mambo yatakayoangaliwa ni kuweka njia kuelekea suluhisho la kisiasa wa mgogoro wa nchi hiyo na kupata uongozi unaokubaliwa na pande zote.

Hata hivyo, Maelezo ya kina kuhusu ajenda ya mazungumzo hayo bado hayajawekwa hadharani.

Libya, ambayo ina utajiri wa mafuta barani Afrika, imekumbwa na vita karibu muongo mmoja, tangu kuangushwa na kuuawa kwa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo Muammar Gaddafi.

**DW.**

## Mashambulizi ya Azerbaijan yawauwa watu 3 mjini Karabakh

RAIA watatu wameuawa baada ya wanajeshi wa Azerbaijan kuushambulia mji mkuu wa mkoa wa Nagorno-Karabakh, jana asubuhi.

Vita kati ya nchi za Armenia na Azebairjan, imetimia imedumu kwa kipindi cha mwezi sasa wakigombea jimbo hilo la milimani.

Msemaji wa wizara ya ulinzi ya Armenia, Shushan Stepanyan, alichapisha picha zinazowaonyesha wafanyakazi wa uokozi wakiondoa vifusi kutoka kwenye jengo moja mjini Stepanakert ambalo liliporomoshwa na makombora.

Wapiganaji wa Kiarmenia wanaotaka kujitenga walikuwa wakikabiliana na wanajeshi wa Azerbaijan, ambao wanapambana kuukamata na kuudhibiti mkoa huo ulijitangazia uhuru wake kufuatia vita vya miaka ya 1990. Mapigano hayo yanaendelea licha ya juhudi za Ufaransa, Urusi na Marekani kutafuta suluhu ya kudumu na hatimaye kusitisha mapigano.

**DW.**

## Corona yaendelea kulisakama bara la Ulaya

UJERUMANI imethibitisha maambukizi mapya ya virusi vya corona 21,000, idadi ambayo imevunja rekodi kutokea kwa siku moja nchini humo.

Katika kukabiliana na wimbi la pili la ugonjwa huo wa Covid-19, nchi nyingine za Ulaya ziliongeza hatua za kupambana na kupanda kwa idadi ya maambukizi kwa kutoa kanuni kali.

Taasisi ya udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza nchini humo ya Robert Koch, ilisema idadi ya visa vipya ilifikia 21,506 kwa kipindi cha saa 24, kutoka 19,000 kwa siku iliyopita.

Hadi asubuhi ya jana, Ujerumani ilithibitisha visa 619,000 tangu kuzuka kwa janga hilo kuibuka kwa mara ya kwanza, huku vifo vilikuwa 11.096.

Ingawa hali hiyo inazidi kuleta hofu serikali ya Ujerumani, nchi nyingine za Ulaya zinatajwa kuwa katika hali mbaya zaidi.

Uingereza ilianza kutekeleza hatua za kudhibiti maambukizi ikiwa ni pamoja kuweka amri ya watu kubakia nyumbani.

Ufaransa, kwa upande mwinginne jana ilianza kupiga marufuku biashara ya migahawa na huduma ya chakula cha kufungiwa pamoja na uuzwaji wa pombe kuanzia saa nne usiku hadi saa 12 asubuhi.

**DW.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**MATHEMATICS TUITION.** Mlete kijana wako tufuatilie msingi wake wa hisabati hadi pale shida ilipoanzia na kuanza kuujenga tena upya. Wahusika ni kuanzia darasa la tano hadi kidato cha sita.Tuitions za majumbani zinapatikana pia. Tupo Bunju Mwisho Dsm. Simu 0655.0754 617987 na 0782 461858

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA VYETI



115984802

**RAYMOND RONALD KIWIA,** Amepotelewa na result slip na leaving certificate ya kidato cha sita yenye index namba S 0534/0574 iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary st ANTHONY , yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **DAR/URA/RB/782892/2020**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



115983202

**SHABAN FIKIRI JUMANNE** anatangaza kupotelewa na result slip yenye No **S.0657/0107** kilichotolewa na NYANSHENYE SECONDARY SCHOOL mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/754489/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ESAU L. SATULO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI KIGLION NYEUSI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC **265CRR,** CHASIS NAMBA **LZL15P901LHH48082.** INGINE NAMBA **KL162FMJ*200848082*** YEYOTE ATAKAYEOINA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI: **MAN/BAB/RB/778007/2020.**

115984902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BERNAD KAKONGI TAYEBWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI **T247CD263** CHASSES NO **MCU150105305** ENGINE NO **IMZ0855330** TOYOTA HARRIER YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**ARU/ARU/RB/782921/2020**

115984502

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA JUDICIARY**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA**

**TAXATION CASE NO. 20/2019**

**(Arising from land case appeal no. 18/2019 of the RMS court Bukoba extended jurisdiction)**

**MURSHID ATHUMAN MUSHULE ...............DECREE HOLDER**

**VERSUS**

**MKAMA PHILIPO .....................JUDGEMENT DEBTOR**

**TO MKAMA PHILIPO**

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Decree holder lodged Application against you and registered as Taxation case no. 20/2019.

Take Notice that the above said application has been fixed for mention on 18th November 2020 at 8:30 am before Hon. J.M. MINDE DR you are ordered to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said hearing the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of this Court this 6th day of Noember, 2020

J.M. Minde
DEPUTY REGISTRAR
BUKOBA

115985002

## KUPOTEA KWA CHETI



11159842O2

**ROINA E KAMWELA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0286/0057** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari **JAMES SANGU GIRL'S** mwaka 2016,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi tarifa **MBE/MBE/RB/439129/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**THOMAS KITURETE SIMEON** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MITSUBISH yenye namba za usajili **T 322 CPU** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi

**MBE/MBE/RB/779462/2020**

115984302

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**GOTARD SALUM IPANDE** amepotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajiri **T 804 CCJ.** Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote Cha polisi. Rb namba

**MOR/MOR/RB/747866/2020.**

115983602

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT BUKOBA**

**CIVIL APPEAL NO 2/2019**

**(Arising from civil case no 14/2015 at Muleba district court)**
**GEORGINA ANGELO.......................APPELLANT**

**VERSUS**

**KHALID SWALEHE AND 9 OTHERS...........RESPONDENT**

**TO, 1.KHALID SWALEHE 2.MBARAKA SHABAN**
**3.FALJARA HUSSEIN 4.SALUM MAHAMUD**
**5.MWOMBEKI EDMUND 6.RAJABU ISSA**
**7.OSWARD CORNEL 8.JUMA HARUNI**
**9.FAIDHAT ATHANASI 10.CHRIZOSTOM SEBASTIAN**

**RE;NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Appellant has lodged a case registered as Civil appeal no 2 of 2019 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 11 th day of November,2020 at 09:00 am before Hon.Judge L.G KAIRO.Your are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 25 th day of Septemba,2020

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

115983802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ALEX ALOYS NG'ASI** Anatangaza kupotelewa kwa kadi za gari aina ya **MITSUBISHI ROSA** namba za usajili **T 723 BWW** na **TOYOTA CAMRY T 859 AQB** yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa

**DAR/MSI/RB/768655/2020**

115984702

## KUPOTEA KWA VYETI



115983502

**MARTINE SYLVESTER MAGUTU,** Amepotelewa na vyeti,cha kidato cha nne index No **S 1470/0134** kilichotolewa na shule ya secondary KIARA mwaka 2009,kidato cha sita index No S **0134-0718** mwaka 2012 shule ya MOSHI secondary, cheti cha chuo na transcript BSC. Agriculture engineering chuo cha( SUA) SOKOINE UNIVERSITY,yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote ch polisi, Polisi taarifa **MSV/RB/458/2020,** Namba ya simu **0789349958.**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT BUKOBA**

**CIVIL APPEAL NO 3/2019**

**(Arising from civil case no 13/2016 at District Court of Muleba)**
**MAULID YAHYA.......................APPELLANT**

**VERSUS**

**1.MUGISHA RENATUS................................RESPONDENT**
**2.ANDERSON CRONEL...............................RESPONDENT**
**3.EVODIUS MICHAEL................................RESPONDENT**
**4.STAVION SELESTIN................................RESPONDENT**
**5.DICKSON RAULIAN.................................RESPONDENT**

**TO, 1. MUGISHA RENATUS**
**2. ANDERSON CRONEL**
**3. EVODIUS MICHAEL**
**4. STAVION SELESTIN**
**5. DICKSON RAULIAN**

**RE;NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Appellant has lodged a case registered as Civil appeal no 3 of 2019 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 23 th day of November,2020 at 09:00 am before Hon.Judge L.G KAIRO.Your are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 12 th day of Octoba,2020

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
BUKOBA

115983902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO.**

**Usimamizi wa mirathi No;312/2020**

**Ombi la SEMENI SHOMARI KIBEGULA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu YOHANA COSMAS MHANGA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/11/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115983702

## LOSS OF CERTIFICATE

**SEASALT LTD** wishes to inform the General public of the loss of its **certificate of incentives no 024415** issued by Tanzania investment centre (TIC) Whoever finds it should report to nearest police station quoting control number **9910819582973**

115983302

**MAHAKAMA YA ARDHI NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO. 203/2020**

**DEBORA RAMADHANI NYAMIZI........................................MDAI**
**Versus**
**EMMANUEL JORAM KASEKWA..................................**
**FINCA MICROFINANCE LTD ..........................MDAIWA**
**PETER MUHEZYA ......................................................**

**YAH KUITWA SHAURINI**

**KWA: EMMANUEL JORAM KASEKWA**

Fahamu kwamba DEBORA RAMADHANI NYAMIZI amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 30/11/2020 saa 3:00 asubuhu mbele ya Mh. A. Mapunda Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kkukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya Mjini.

**Kumbuka:** usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 04/11/2020

A. Mapunda
MWENYEKITI
04/11/2020.

115983102

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.


# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.
Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.
Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.
Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini-37

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**




"Kwa nini mnataka kumuua binti yenu?"

George alikaa kimya na kutafakari. Alikuwa kama mtu anayesali hivi. Baada ya dakika tano aliinua macho.

"Nisamene bwana mkubwa, ngoja niseme kitu ambacho kitarahisisha yote haya."

Maneno hayo yalimshangaza Timo na msaidizi wa Eddy, lakini mwenyewe Eddy alijua kuwa George atazunguka, lakini hakuna na ujanja kama ni kweli amefanya hivyo. Na kama si kweli, basi atakuwa anamjua mtu ambaye yuko nyuma ya hayo yote.

"Tatizo hapa ni mali tu. Kuna baadhi ya ndugu zangu baada ya kifo cha Patiyo ambaye alikuwa na mali nyingi na kampuni, waliona hakuna haja ya kumuachia binti mali, kwani mama yake mzazi alifariki wakati bado mdogo. Kwa maana hiyo mali ile ni yake. Kaka yetu mkubwa anaitwa Jim, ndiye aliyetuita na kupanga mkakati wa kumuua Shani ili mali zile sasa zote zitahamia kwetu kwa sababu hakutokuwa na mrithi nwingine yoyote, kwani binti ni mtoto pekee wa marehemu." Alisema Gaorge na kushusha pumzi kana kwamba ameutua mzigo mzito.

"Mpango huu ulianza kabla ya kifo cha Patiyo au baada?"

"Kwa sababu nimeamua kukueleza ukweli, bado nitaendelea kueleza ukweli. Ilikuwa ni baada ya kifo cha Patiyo."

"Hamkuhusika kumuua Patiyo ili baadaye mfanye hivyo kwa binti yake?"

"Hapana." Alisema George akionekana kuwa na uhakika na anachokisema.

"Sisi hatukuhusika na njama za kumuua Patiyo na mkewe wakati wakifunga ndoa. Wazo la kumuua Shani lilikuja baada ya ndugu yetu kufariki na hii ni baada ya mazishi, kikao cha familia, halafu kaka yetu Jim aliitisha kikao cha sisi tu wanaume na kutueleza mpango huo."

"Kwenye mpango huo mlikuwa wangapi?"

"Wanne, kaka yetu Jim, mimi, Paul na Ben."

"Sasa nataka kitu kimoja. Utusaidie ili ndugu zako wote hao wapatikane. Na ikiwa hivyo unaweza kupata unafuu wa adhabu. Badala ya kukupa mashataka ya kujaribu kuua kwa makusudi kama wenzako, wewe naweza kuwaambia wakufungulie mashtaka ya kujaribu kuua bila kukusudia. Sawa?"

"Sawa."

"Hebu nisaidie kitu kimoja, kwa nini hamkutumia risasi kumuua Shani, mkataka kutumia sumu, tena inayoua taratibu?" Eddy alimrudia tena George kwa maswali.

"Kumbuka mheshimiwa kuwa sisi si wauaji, ila ni tamaa ya mali, na hasa kaka yetu Jim, kwa hiyo baada ya majadiliano marefu tukaamua hivyo. Kwanza angekufa kwa risasi au ghafla, wengi wangekuwa wasiwasi na sisi na huenda uchunguzi ungeanza, kwa hiyo tukaamua kumuua kwa sumu inayoua taratibu kwa kumtumia Fikiri ambaye tukampa shilingi milioni moja za kwanza na aliuawa kabla hajapata milioni moja nyingine. Na tulifanya hivyo ili tusitoea ya pili, pia kuficha ushahidi kwa sababu angekamatwa tu, tungekuwa hatiani."

****************************

Wiki moja baadaye tayari Paul alikuwa ametiwa mbaroni. Sasa walikuwa wamekamatwa wawili. George na Paul. Jim na Ben walifanikiwa kutoroka. Hawakujulikana waliko. Eddy ndiye aliyemwagiza msaidizi wake kuwaambia askari polisi wawakamate Jim, Ben na Paul. Hata hivyo kwa namna ya ajabu Jim na Ben hawakupatikana.

Ni kwamba walihisi hatari. Kitendo cha ndugu yao George kukamatwa na kukaa wiki moja akiwa kizuizini kiliwafanya wajiongeze. Hawakutarajia kesi ya gari kuendeshwa na mtu aliyefanya kosa la barabarani kukaa wiki nzima.

Waliona kuna namna. Wakawa hawalali nyumbani kwao. Na hata siku askari walipokuja majumbani kwao kuwakamata wakaisaidie polisi, hawakuwa sehemu ya watu waliolala nyumbani kwao siku hiyo.

Ben, alipobanwa na yeye, maelezo yake hakupishana sana na ya George. Ndipo Eddy alipogundua kuwa ndugu wale walichotaka ni kumuondoa duniani Shani kwa ajili ya kuchukua na kugawana mali za marehemu kaka yake Patiyo Kupila ambaye hakuwa na mtoto yoyote zaidi ya Shani. Kifo cha Shani kingesababisha kisheria mali irudi kwao kama ndugu kwa sababu marehemu pia hakuwa na mke. Mke wake wa kwanza alifariki muda mrefu uliopita. Wakati huo Shani bado mdogo. Aliishi miaka mingi bila mke kwa sababu hakutaka binti yake aishi na mama wa kambo wakati akiwa mdogo. Binti yake alipofika miaka 23, akaamua kuoa. Alimuoa Grace Patiyo ambaye Eddy ni shangazi yake. Ni mtoto wa mwisho kuzaliwa kwenye familia ya baba yake mzazi mzee Kamal. Wakati wa harusi yao alikuwa nchini Marekani. Waliuawa siku hiyo hiyo waliofunga ndoa.

Sasa rasmi akajua kuna makundi mawili. Moja ni lile lililomuua Patiyo na mkewe Grace kwa sababu zisizojulikana na hili la kina Jim ambalo lengo lao ni mali za ndugu yao.

Tayari aliona kundi la kina Jim alikuwa amelidhibiti kirahisi sana. Tangu alipookota kifuko cha sumu kwa marehemu Fikiri ambacho alipewa na ndugu hao kwa ajili ya kumuua Shani ambaye kisheria alikuwa ndiyo kikwazo kwao kuchukua mali.

Lakini hadi leo hakujua au lau kupata fununu za aliyewaua Patiyo baba mzazi wa Shani na mkewe Grace ambaye ni shangazi yake. Kundi hili ndilo aliliona ni gumu zaidi kwani mpaka sasa halijaacha nyayo yoyote ile nyuma.

****************************

"Mpenzi, nimepata taarifa kuwa baba zangu wadogo George na Paul wamekamatwa." Sauti ya Shani ilipenya kwenye masikio ya Eddy. Ilikuwa ni muda mfupi tu baada ya kuwasili nyumbani kwao Kijitonyama.

Shani na Eddy sasa waliishi pamoja. Ni baada ya tukio la Mbezi Beach ambalo watu wawili walivamia kwenye nyumba ya Shani kwa nia ya kutaka kumdhuru kwa kutumwa na Jim na ndugu zake.

"We nani kakupa hiyo taarifa?" Eddy aliuliza kwa mshangao.

"Mama mdogo Marina, mke wa George kaniambia kuwa mumewe ana wiki sasa amekatwa, na tayari baba mdogo Ben amekamatwa na yeye."

"Mmmh, kwani wamefanya nini hadi wakamatwe mtu na ndugu yake?" Eddy alihoji kinafiki kwani alifahamu kila kitu na yeye ndiye mhusika mkuu wa kuwatia wote hao mbaroni.

"Mwenzangu, hata sielewi, halafu nimeambiwa kuwa baba mkubwa Jim na Ben hawaonekani nyumbani, sijui imekuwaje?" Shani alilalama kwa namna ya masikitiko.

"Labda na wao watakuwa wamekatwa ila vituo tofauti, inabidi na wao watafutwe kwenye vituo vingine."

"Inawezekana eee, kweli wewe umesema, ngoja nimpigie mama mdogo nimwambie?"

Eddy alimtazama Shani jinsi alivyokuwa amehamanika kutokana na baba zake wadogo na wakubwa kukamatwa.

"Laiti angejua kuwa mimi ndiye niliyetoa amri ya kuwatia mbaroni? Laiti angekua kuwa kosa lao ni kutaka kumuua yeye ili wachukua utajiri wa baba yake..." Eddy alijisemea moyoni huku akimtazama kwa makini Shani.

"Mbona kama unanishangaa sana Eddy?" Aliuliza.

"Umependeza."

"Yaani huko kote hukuniambia, uje kuniambia huku."

"Sikutaka watu wasikie ninavyokusifia."

Siku zote Shani anafahamu kuwa Eddy ni mtu wa mzaha. Akamuacha kama alivyo, huku akitabasamu.

Kama kawaida Eddy aliifanya kazi yake kwa ustadi mkubwa. Mpaka sasa, pamoja na kuwa wote kama wapenzi, lakini Shani alikuwa hajagundua kuwa anaishi na mpelelezi mashuhuri nchini Tanzania, Eddy Kamal.

Hajagundua kama alikuwa amewekewa sumu kwenye chakula siu ile kule ABC Hotel ili afe taratibu.

Alikuwa hajui chochote kuwa Eddy alimponya kwenye mkasa huo, kiasi cha kusababisha baadaye kifo cha Fikiri aliyepewa kazi ya kuweka sumu.

Alikuwa hajui kuwa waliovamia nyumbani kwake walikuwa na lengo lile lile la kutaka kummaliza. Aliyeelewa hilo ni Eddy pekee. Yeye alidhani ni wezi tu.

Sababu kubwa ya Eddy kufanya hivyo ni kutomtisha. Alitaka msichana huyo aishi kwa amani. Angejua kuwa kuna watu wanamfuatilia wamuue, asikuwa na amani na furara tena. Angejua ndugu zake ndiyo wanataka kumuua, angeshangaa na kukosa raha. Kila ktu alipanga kumaliza yeye kabla ya Shani kudhurika. Ndiyo maana alimtoa Mbezi Beach alikokuwa akiishi na kumleta kwake Kijitonyama.

***Itaendelea Jumamosi***

HABARI MICHEZO



# UPAMECANO

## ANAPITIA WAKATI MGUMU – DESCHAMPS

**PARIS, Ufaransa**

DIDIER Deschamps anaamini Dayot Upamecano anapitia "wakati mgumu" baada ya mlinzi huyo kuachwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Deschamps amesema nyota huyo wa RB Leipzig, Upamecano mwenye umri wa miaka 22 ambaye ameichezea mechi tatu Ufaransa, anaweza kupata nafasi kwa siku za usoni.

"Kuna ushindani mkubwa katika nafasi hii. Alikuwa na sisi hapo kabla. Anapitia wakati mgumu kwa sasa," alisema kocha huyo wa Ufaransa akiwaambia waandishi wa habari.

"Anajua anaweza kufanya vizuri zaidi. Alikuwa mtulivu Septemba wakati tulipomwita kwa mara ya kwanza na Oktoba. Ni kijana mdogo na ana nafasi nzuri tu. Anacheza mechi nyingi.

"Bila shaka kama sio yeye ni mwingine, ni kuhusu ushindani. Kurt Zouma ambaye anafanya vizuri kule Chelsea anaijua vizuri Timu ya Taifa ya Ufarasa.

"Mlango haujafungwa. Nimefanya uchaguzi huo leo kwa sababu maalumu. Na inaweza kuwa hivyo hivyo kwa Machi na Juni?

"Ni jambo la kawaida kwa wachezaji wote ambao hawajaitwa, lakini wanaweza kuwa na matumaini ya kuitwa tena kwenye timu ya taifa."



## ARTETA ATAKA KIWANGO ZAIDI KWA PEPE

**LONDON, England**

MIKEL Arteta bado anataka ubora mwendelezo kutoka kwa Nicolas Pepe baada ya mshambuliaji huyo kufunga wakati wakishinda mabao 4-1 kwenye Ligi ya Europa dhidi ya Molde, juzi Alhamisi.

Pepe alifunga na kutoa pasi ya mwisho wakati Arsenal ilipojivuta kileleni mwa msimamo wa Kundi B.

Nyota huyo wa kimatafa wa Ivory Coast, ambaye alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 72 mwaka jana, ana mabao mawili na pasi za mwisho mbili kwenye Ligi ya Europa msimu huu, lakini ameanza katika mechi moja tu kwenye Ligi Kuu England.

Na sasa kocha wa Arsenal, Arteta anataka Pepe kuendelea kuwa kwenye kiwango bora zaidi wakati watakapocheza na Aston Villa kwenye Ligi Kuu, Jumapili.

"Kiwango mwendelezo katika kila mchezo, kwa dakika zote 90, katika kila mchezo, na naamini anaweza kufanya vizuri zaidi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunahitaji zaidi uwezo wake kwa sasa. Alifunga bao bora na kutoa pasi ya mwisho na anaweza kufanya mengi zaidi uwanjani.

"Kiujumla anatakiwa kuwa kwenye kiwango chake katika mchezo, katika kila wiki na kwenye mechi zote."


## MADDISON: NIMESIKITIKA KUACHWA ENGLAND

**LONDON, England**

JAMES Maddison amekubali amekatishwa tamaa kwa kuondolewa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England, lakini ameahidi kupambana ili arejeshwe kwenye kikosi hicho.

Gareth Southgate alithibitisha kikosi chake kitakachoivaa Ireland, Ubelgiji na Iceland, lakini hakumwita nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, wakati akitangaza kikosi hicho juzi Alhamisi.

Maddison kwa sasa hajajumwishwa kwenye kikosi hicho tangu alipoitwa kwa mara ya kwanza kwenye mchezo dhidi ya Montenegro



uliofanyika Novemba, mwaka jana.

Alipoulizwa kama alijisikia vibaya kwa kuondolewa kwenye kikosi hicho, Maddison nyota wa Klabu ya Leicester City aliiambia BT Sport: "Ndio, nimejisikia vibaya.

"Nataka kuwa kwenye kikosi cha England, hicho ndio nilichokiota tangu ututoni. Napenda kuichezea timu yangu ya taifa.

"Niko fiti, lazima nipambane kuhakikisha naitwa tena kwenye kikosi hicho. Nilikuwa na majeruhi kwa muda mrefu.

"Kwa sasa nahitaji kupambana kwa nguvu zaidi ili niweze kurudi kwenye timu hii, maana nataka kutimiza ndoto yangu ya muda mrefu."



# WILLOCK

## AAHIDIWA NAFASI ARSENAL

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amemhakikishia, Joe Willock nafasi yake kwenye Ligi Kuu England itakuja, endapo kiungo huyo ataendelea kuwa na kiwango bora kama alichokionyesha wakati Arsenal ikishinda 4-1 dhidi ya Molde kwenye Ligi ya Europa.

Willock alifunga bao la mwisho kwa washikabunduki hao na alitengeneza moja kati ya mabao mawili ya kujifunga ya Molde.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 hajacheza mchezo wowote kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Na sasa Arteta amesema kwamba, Willock anaweza kucheza mechi nyingi zaidi kama ataendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi.

Bosi huyo wa Arsenal aliambia BT Sport: "Joe Willock angeweza kufunga mabao mengi zaidi, alitengeneza goli na alikuwa kwenye kiwango bora kabisa.

"Kama ataendelea kuwa kwenye ubora huu atakuwa na nafasi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu."

## KOCHA MILAN ALIA NA KICHAPO EUROPA

**MILAN, Italia**



STEFANO Pioli anaamini AC Milan walijisababishia matatizo yao wenyewe wakati walipochapwa 3-0 nyumbani na Lille kwenye mchezo wa Ligi ya Europa.

Yusuf Yazici alifunga mabao yote matatu 'hat-trick' ikiwa ni kwa mara ya kwanza mchezaji mmoja kuifunga idadi hiyo ya mabao Milan nyumbani kwao, tangu alipofanya hivyo, Rivaldo wakati akiichezea Barcelona Oktoba, mwaka 2000.

Kipigo hicho cha Milan kilikuwa kimemaliza mwendelezo wao wa kutofungwa mechi 24 kwenye mashindano yote.

Lille imekuwa timu ya kwanza kuifunga Milan tangu Genoa walipofanya hivyo Machi kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Yazici mwenye umri wa miaka 23 amekuwa mchezaji wa kwanza kwenye historia ya mashindano hayo ya Ulaya kufunga 'hat-trick' mara mbili ugenini kwa msimu mmoja, alifunga dhidi ya Sparta Prague, Oktoba, mwaka huu.

Pioli akabainisha baada ya mchezo huo kuwa Milan ilijitengenezea matatizo yenyewe na kwamba hawana wa kumlaumu.

"Tulicheza dhidi ya timu imara zaidi ya sisi na ilikuwa wakati mgumu zaidi kwa sisi wenyewe," amesema Pioli akiiambia Sky Sport Italia.

"Hatukuanza vibaya, lakini nilifikiri kwamba tungekuwa hatari zaidi kwenye mashambulizi, lakini tukashindwa kutengeneza nafasi za kutosha ili kupata mabao."



## MARADONA AKARIBIA KURUHUSIWA HOSPITALI

**BUENOS AIRES, Argentina**

AFYA ya nyota mkongwe, Diego Maradona imeimarika na anaendelea vizuri baada ya kufanyiwa oparesheni ya ubongo na anaweza kuruhusiwa kuondoka hospitali wakati wowote, kwa mujibu wa daktari wake binafsi, Leopoldo Luque.

Gwiji huyo wa Argentina alifanyiwa oparesheni ya kuondoa damu iliyovuja kwenye ubongo Jumanne, baada ya kukimbizwa hospitali wakati akiwa hajitambui.

Luque amebainisha afya ya Maradona, ambaye ana umri wa miaka 60 imekarika zaidi.

"Anaendelea vizuri na afya yake imeimarika vizuri sana," aliwaambia waandishi wa habari katika hospitali ya Olivos Clinic iliyopo jijini, Buenos Aires, ambapo Maradona amelazwa.

"Kwa sasa anaweza kuruhusiwa kuondoka wakati wowote. Anajiona kama vile tayari anaweza kuruhusiwa.

"Kwani anaweza kutembea, anazungumza na mimi, yuko vizuri kabisa na anajiona yupo tayari kurudi nyumbani."

Maradona, ambaye alishinda Kombe la Dunia na Argentina mwaka, 1986 na kuiwezesha Napoli kushinda mataji mawili ya Ligi Kuu Italia, Serie A, alianza kuinoa klabu ya Ligi Kuu Argentina, Gimnasia ya Esgrima La Plata tangu mwaka 2019.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YATAMBA ITAMNASA HAALAND

●●●Yaeleza imejiimarisha kumsajili mshambuliaji huyo wa Dortmund ifikapo mwaka 2022...

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid imepanga kuhakikisha inamnasa nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland ifikapo mwaka 2022, kwa mujibu wa ukurasa wa mbele wa gazeti la AS lililochapishwa jana Ijumaa.

Haaland mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akitajwa kama mmoja wa washambuliaji bora Ulaya wakati akiendelea kutamba.

Na sasa Real Madrid imeweka mipango yake kuhakikisha inamsajili nyota huyo wa kimataifa wa Norway.

Kwa mujibu wa AS, Real Madrid watatumia nguvu yao yote ili kumtwaa mshambuliaji huyo ambaye amekuwa pia akihusishwa na klabu nyingi kubwa barani Ulaya.

Haaland amefunga mabao 10 katika mechi 10 za mashindano yote kwa Dortmund msimu huu.

Imeripotiwa kwamba, wakala wa nyota huyo wa zamani wa Klabu ya Salzburg, Mino Raiola - ameshafikia makubaliano na Dortmund na inaelezwa nyota huyo ataondoka pale BVB mwaka 2022, ingawa ada yake bado haijawekwa hadhrani.

Haaland ameanza msimu wa 2020-21 kwa ubora zaidi akifunga mabao matano kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ambapo msimu uliopita alifunga mabao 13 katika mechi 15 alizoichezea Dortmund.

## KWA UFUPI

**UNITED YAMFUATA POCHETTINO**

KLABU ya Manchester United imezungumza na kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino kuhusu kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer pale Old Trafford. ***(MEN)***

**SOLSKJAER HALI TETE**

NAFASI ya Kocha, Ole Gunnar Solskjaer kwenye kikosi cha Manchester United ipo katika hatihati baada ya vipigo mfululizo na tayari kuna tetesi za kufukuzwa endapo timu hiyo itakubali kufungwa leo na Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England. ***(Star)***

**SON KUVUNA DONGE NONO**

MWENYEKITI wa Klabu ya Tottenham Hotspur, Daniel Levy ametoa ofa kwa mshambuliaji, Son Heung-min, ambaye ana umri wa miaka 28 ya kupata mshahara sawa na nahodha, Harry Kane likiwa ni jaribio la kuhakikisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini anasalia katika klabuni hapo. ***(Express)***

**THURAM AGOMBEWA ULAYA**

KLABU za Manchester City, Barcelona na Juventus, zinamfuatilia mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach, Marcus Thuram ambaye ana umri wa miaka 23 pamoja na Alassane Plea (27). ***(Bild)***

**MADRID, POGBA KITAELEWEKA**

REAL Madrid huenda ikamsajili kiungo wa kati raia wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, kutoka Manchester United kwa kitita cha pauni milioni 54 ifikapo msimu ujao. ***(AS)***

**ELNENY ATAKIWA ARSENAL**

KLABU ya Arsenal inajiandaa kujadili kuhusu kuongeza mkataba wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Elneny, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Mail)***

**SCHALKE KUMWACHIA KABAK**

KLABU ya Schalke inaweza kuridhia kumruhusu beki wa kati Mturuki, Ozan Kabak mwenye umri wa miaka 20, kuondoka kwa pauni milioni 18 ifikapo Januari mwakani. Nyota huyo anatajwa kuwaniwa na mabingwa wa England, Liverpool. ***(Bild)***

**LIVERPOOL ILIMKATAA JOTA**

DIOGO Jota mwenye umri wa miaka 23, alikuwa mbadala kwenye dirisha la usajili na winga wa Watford, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 22 raia wa Senegal. ***(Mirror)***

**BOLASIE, GROSICKI SOKONI**

KOCHA wa Middlesbrough, Neil Warnock, anafikiria uwezekano wa kuwanasa wachezaji wawili, kiungo wa kati wa Poland anayekipiga West Brom, Kamil Grosicki na Yannick Bolasie (31). ***(Northern Echo)***

**BOSI AONDOKA ARSENAL**

MKUU wa Idara ya maendeleo ya makocha na wachezaji wa Arsenal, Marcel Lucassen, anajiandaa kuondoka klabuni hapo kwa sababu zake binafsi. ***(The Athletic)***

**BOWYER ANUKIA WEST**

WEST Brom inaangalia uwezekano wa kumwajiri, Lee Bowyer, ambaye alikuwa kocha wa klabu inayoshiriki League One ya Charlton, kama itaendelea kuwa na matokeo mabaya chini ya Slaven Bilic. ***(Mirror)***

**BERBATOV AFUNGUKA**

STRAIKA wa zamani wa Manchester United, Dimitar Berbatov amesema ni vigumu kulaumu namna ambavyo klabu hiyo inavyotaka kumwajiri Mauricio Pochettino kuwa kocha mpya kutokana na presha inayomzunguka, Ole Gunnar Solskjaer.

HABARI MICHEZO

# MPINZANI WA MWAKINYO ATUA, AANZA MAJIGAMBO

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA Jose Carlos Paz kutoka Argentina ambaye anatarajiwa kuzichapa na Hassan Mwakinyo katika pambano la kuwania mkanda wa dunia wa WBF uzito wa Super Welter litakalofanyika Novemba 13, mwaka huu Ukumbi wa Next Door Arena jijini, Dar es Salaam amewasili nchini na kutamba atafanya vyema kwenye mtanange huo.

Mwakinyo kutoka jijini Tanga ndio bondia anayeshikilia mkanda huo.

Paz amewasili na baba yake, Alberto Ramon Paz ambaye pia ni kocha wake kama ilivyo kwa bondia, Floyd Mayweather.

Akizungumza mara baada ya kutua nchini juzi usiku, Paz alisema amesafiri umbali mrefu kwa ajili ya kuufuata ubingwa wa pambano hilo linalojulikana kwa jina la Jackson Group Fight Night.

Paz alisema amechukua tahadhari kubwa kwa ajili ya kupambana na Mwakinyo kwa sababu anafahamu bondia huyo mwenyeji ana rekodi nzuri.

Alisema alianza mazoezi kwa muda mrefu kwa ajili ya kushiriki pambano na amepanga kuweka rekodi mpya akipigana kwa mara ya kwanza hapa Tanzania.

"Nimefika mapema zaidi ili kuzoea hali ya hewa, hii ni moja ya mikakati ya ushindi, nilisafiri kwa basi na baadaye kupanda ndege, siku mbili nipo njiani, sitakuwa tayari kushindwa katika pambano hili," alisema Paz.

Kocha wake, Alberto alisema wamemsoma Mwakinyo katika mapambano yake yaliyopita na kujua mbinu zake ambazo amezifanyia kazi.

"Tumefanya mazoezi magumu kuelekea pambano hili, tumefanya mazoezi ya ufundi na mbinu, hayo yote ni kwa ajili ya kusaka ushindi ambao tunaamini tutaupata kwa asilimia 100, tutashinda," alisema Ramon.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na mabondia kutoka Zambia, Zimbabwe na Kenya watawasili wiki ijayo kwa ajili ya pambano hilo.

Twissa alisema kila kitu kiko katika hatua za mwisho na tiketi zitaanza kuuzwa kwa njia ya mtandao wa Nilipe na Selcom kwa Sh. milioni tatu kwa meza ya watu 10 na Sh. 150,000 kwa kwa viti vya kawaida.

Alitaja mapambano ya utangulizi yatakuwa matatu ambapo, Zulfa Macho atacheza dhidi ya Alice Mbewe wa Zambia wakati Hussein Itaba atazichapa na Alex Kabangu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Fatuma Zarika wa Kenya atachuana na Mzimbabwe, Patience Mastara.




Bondia, Jose Carlos Paz kutoka Argentina (wa pili kulia) baada ya kuwasili nchini kwa ajili ya kushiriki pambano la kuwania mkanda wa uzito wa Super Welter (WBF), dhidi ya bingwa mtetezi, Hassan Mwakinyo litakalofanyika wiki ijayo. Wengine ni baba na kocha wake, Ramon Paz ( wa pili kushoto), Mwakilishi wa Jackson Group Sports, Don Hala (kushoto) na Katibu Mkuu wa Kamisheni ya Ngumi za kulipwa nchini (TPBRC), Yahya Poli. **PICHA: MTANDAO**

# Tigo yazawadia washindi 100

**Na Faustine Feliciane**

WASHINDI 100 wa promosheni ya 'Jaza Tukujaze Tena' inayoendeshwa na Kampuni ya huduma za simu ya mkononi ya Tigo wamejinyakulia simu za kisasa 100 katika mwanzo wa kampeni ya promosheni hiyo.

Aidha zaidi ya wateja milioni nne wamepokea bonasi ya zawadi mbalimbali kutoka katika kampuni hiyo.

Akizungumza jijini, Dar es Salaam jana wakati wa kukabidhi zawadi hizo, Meneja wa Kitengo cha Bidhaa cha kampuni hiyo, Suleiman Bushagama, alisema tangu walipozindua kampeni hiyo Oktoba 23, mwaka huu tayari wametoa mamilioni ya dakika za bure kwa wateja wao.

"Mbali na dakika milioni 149 tulizotoa, MB za data milioni 504 na SMS milioni 81 kwa wateja wetu nchi nzima ambao walinunua vifurushi tangu kuzinduliwa kwa kampeni hii," alisema Bushagama.

Pia alisema ili wateja wapokee ofa za papo hapo, wanapaswa kununua aina yoyote ya kifurushi katika huduma zao.

Kwa upande wake, mmoja wa washindi wa promosheni hiyo, Frank Lyakurwa, ambaye ni mstaafu, kutoka Madale jijini amejishindia simu janja ya Samsung Note 20 huku akielezea kufurahia ushindi huo.

"Kwanza niseme tu sikuamini nilipoambiwa taarifa za ushindi wangu, nilinunua bando la internet la wiki kwa Sh. 3,000 ambapo nilipewa bonus ya GB 2, baada ya hapo nilipigiwa simu kwamba nimejishindia Samsung Note 20. Sikuamini," alisema Lyakurwa.

Mshindi mwingine, Jorum Mwakipesile, mkazi wa Shinyanga alisema amefurahi kujishindia simu aina ya Itel T20 baada ya kununua bando la Sh. 500.

Katika hatua nyingine, kampuni ya simu ya Tigo Tanzania imewatahadharisha wateja wake wote na Watanzania kwa ujumla kuwa makini na matapeli wanaoweza kuibuka kupitia mgongo wa promosheni hiyo.

## Biashara yajipanga kubadilisha kikosi

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inarejesha makali yake, Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza amesema anajiandaa kubadilisha kikosi chake ili kurejea kwenye kasi ya ushindi katika mechi za Ligi Kuu Bara zitakazofuata.

Baraza ametoa kauli hiyo baada ya kupoteza pointi tano nyumbani katika mechi mbili zilizopita na hivyo kumfanya ajipange upya.

Kocha huyo alisema amejiandaa kubadilisha mfumo ili apate pointi sita au nne za ugenini atakapowafuata Dodoma Jiji FC na Kagera Sugar.

Alisema tayari ameanza kuyafanyia kazi upungufu uliojitokeza ili kuhakikisha anarejea kwenye ushindani kwa kuwatumia nyota wake wawili wa kigeni ambao ni kiungo mshambuliaji, Christian Zigger na beki wa kushoto Mkenya, Bolton Omwenga ambao hawajawi kucheza tangu wamesajiliwa katika timu hiyo.

"Nyota hawa wawili hawakuwa na vibali vya kazi, sasa wamepata na watakuwa miongoni mwa wachezaji ambao wataingia katika mabadiliko ya kikosi changu, na wengine ambao hawakupata nafasi ya kucheza mara kwa mara katika mechi zilizopita," alisema Baraza.

Aliongeza licha ya kupangua kikosi chake lakini pia atakuwa makini katika kubadilisha mbinu kama alivyofanya katika mechi dhidi ya Polisi Tanzania na Coastal Union ambazo walicheza ugenini.

## Uchaguzi wa Bodi Z'bar wasogezwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesogeza mbele uchaguzi wa Bodi ya Ligi ya shirikisho hilo hadi Novemba 14, mwaka huu kutokana na wadau kushindwa kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Omar Makungu, alisema awali walipanga kufanya uchaguzi huo leo ili kuwahi kalenda ya msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar lakini, imeshindikana.

Makungu alisema kamati hiyo inatarajia kukutana leo ili kupanga siku ya mwisho ya kuchukua na kurejesha fomu kwa wagombea watakaojitokeza lakini ikiwaomba wadau washiriki kikamilifu katika mchakato huo.


"Tumesogeza mbele uchaguzi wa bodi, sasa utafanyika Novemba 14, mwaka huu na sababu kuu ni kutokujitokeza kwa wagombea hadi kufikia leo (jana), mipango mingine tutaitangaza baada ya kukutana kesho (leo) Jumamosi," Makungu alisema.

Kiongozi huyo alisema kamati yake itapanga tarehe nyingine ya kuhakiki fomu za wagombea na baadaye itatangaza majina ya wadau ambao watakuwa wamepitishwa kuwania uongozi wa bodi hiyo.

"Tunawakumbusha viongozi wa timu za Ligi Kuu kujitokeza kuwania uongozi kwa sababu wao wana sifa zilizotajwa katika katiba ya bodi ya ligi, wasisite kujitokeza kugombea nafasi hizo," alisema kiongozi huyo.

Alitaja nafasi zinazowania kwenye uchaguzi huo ni pamoja na mwenyekiti, makamu mwenyekiti, wajumbe wanne (wawili watatoka katika klabu za Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba na wengine wa Kanda ya Unguja).

Michezo
Jumamosi Novemba 7, 2020
Nipashe



MADRID YATAMBA ITAMNASA HAALAND HABARI UK 22



Cedric Kaze



Sven Vandenbroeck

# YANGA, SIMBA SC NI VITA NA WAVULANA, WANAUME

## ●●●Kaze afunguka anahitaji pointi zaidi, wakati Sven akisema 'dabi' itakuwa tofauti...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

MAJIGAMBO na tambo zilizokuwa zikiendelea kutoka kwa wanachama na mashabiki wa klabu za Simba na Yanga zinatarajia kumalizika baada ya timu zao kukutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini. Dar es Salaam.

Ni mechi ya kiporo ambayo awali ilitarajiwa kufanyika Oktoba 18, mwaka huu, lakini ikasongezwa mbele na kusababisha wadau wa timu hizo mbili kuusubiri kwa hamu mchezo huo maarufu kwa jina la 'Kariakoo Dabi'.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema amekiandaa vyema kikosi chake na wamejipanga kupata ushindi bila kujali idadi ya mabao.

Kaze alisema wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo na amewaandaa kutohofia majina ya wapinzani wao.

"Tunaenda kucheza na bingwa mtetezi miaka mitatu imeisha, tunajua ugumu wa mechi ya kesho (leo), ni 'dabi' kubwa sana kwa mashabiki wa kwetu na wachezaji wetu, tunataka kuona kipimo cha wachezaji kama kimegeuka kuliko mwaka jana, ni majaribio makubwa kwetu," Kaze alisema.

Sven Vandenbroeck, Kocha Mkuu wa Simba, alisema mechi ya leo itakuwa ni tofauti na 'dabi' nyingine zilizopita kwa sababu watani zao Yanga wamebadilika.

Kocha huyo alisema wamejiandaa kuondoka na pointi tatu muhimu ili kupunguza tofauti ya pointi nne waliyonayo sasa dhidi ya wapinzani hao kwenye vita ya kuwania taji la Ligi Kuu Bara.

"Yanga wa kikosi kipya, wana kocha mpya, haitakuwa kama mechi zilizopita, lengo lengu ni kushinda na kuwakaribia kwenye msimamo wa ligi," alisema Sven.

Misimu kadhaa nyuma, Simba ilionekana ina kikosi kizuri kuliko Yanga ingawa matokeo wakati mwingine hayakuwa mzuri upande wao, lakini msimu huu wanachama na mashabiki wa Yanga wamekuwa na imani kubwa na kikosi chao kutokana na usajili wa gharama uliofanyika.

Yanga ambayo ndiyo mwenyeji wa mechi ya leo, itakuwa na wachezaji wengi wapya ambao watakuwa wakicheza 'dabi' hiyo kwa mara ya kwanza, mbele ya maelfu ya mashabiki ambao hujazana kwa wingi uwanjani.

Wachezaji hao kama watapangwa ni pamoja na Carlos Carlinhos, Mukoko Tonombe, Tuisila Kisinda, Michael Sarpong, Yassin Mustapha, Zawadi Mauya, Farid Mussa, Waziri Junior, Bakari Mwamnyeto, Kibwana Shomari na Yacouba Songne.

Kwa upande wa mabingwa watetezi, wachezaji ambao wanaingia taratibu kwenye kikosi cha kwanza na ni wapya ni Rally Bwallya, Chriss Mugalu na Joash Onyango. Hata hivyo kati ya wachezaji hawa wapya, mwenye matumaini ya asilimia kubwa kuanza na kumaliza mechi ni Onyango pekee.

Hii ni kwa sababu Simba inategemea kikosi chake kile kile cha msimu uliopita ambacho kwa mara ya mwisho iliichapa Yanga mabao 4-1 kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA, Julai 12, mwaka huu.

Mara ya mwisho kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga iliibamiza Simba bao 1-0, mchezo uliofanyika Machi 8, mwaka huu mfungaji akiwa ni Bernard Morrison ambaye kwa sasa yupo upande wa pili.

Hata hivyo, Simba itamkosa Morrison kwenye mechi hiyo kutokana na kutumikia adhabu ya mechi tatu baada ya kosa la kumpiga beki wa Ruvu Shooting, Juma Nyosso kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa wiki iliyopita.

Simba pia itamkosa straika wake tegemeo, Meddie Kagere ambaye yuko kwao Rwanda akiuguza maumivu ya goti, ingawa taarifa zingine zinasema nyota huyo ameanza mazoezi mepesi na kikosi cha Rwanda ( Amavubi), inayojiandaa kuikabili Cape Verde.

Kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza mzunguko wa kwanza msimu uliopita iliyochezwa Januari 4, mwaka huu, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2.

Iwapo mchezaji yoyote mzawa wa Simba atafunga bao kwenye mechi hiyo ya ligi, basi atakuwa anafanya hivyo kwa mara ya kwanza tangu 2018.

Mchezaji wa mwisho mzawa kufunga bao kwenye 'dabi' hiyo alikuwa ni Erasto Nyoni, alicheka na nyavu dakika ya 37 Aprili 29, mwaka 2018 na Simba kupata ushindi wa bao 1-0.

Tangu wakati huo, mabao ya Simba kwenye 'dabi' za Ligi Kuu yamekuwa yakifungwa na wachezaji wa kigeni, ukiondoa kwenye mechi ya FA, Mzamiru alipofunga bao moja, mengine yakifungwa na Mzambia Clatous Chama na Mbrazil, Gerson Fraga.

Mchezaji yoyote atayefunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye 'dabi' hiyo atakuwa ameweka rekodi iliyowekwa na Abdallah Kibadeni mwaka 1977, alipofanya hivyo Julai 19, mwaka huo, dakika ya 10, 42 na 89, Simba ikiisulubu Yanga mabao 6-0.

Mechi ambayo ilikuwa na matokeo yaliyoshangaza mengi ilikuwa ni ile ya Oktoba 20, mwaka 2013, Ligi Kuu Bara ya msimu wa 2013/14, timu hizo zikifungana mabao 3-3, Yanga ikitangulia kupata mabao matatu kipindi cha kwanza na Simba kusawazisha dakika 45 za pili.

Mabao ya Yanga yalifungwa na Mrisho Ngassa dakika ya 15, Hamisi Kiiza aliyepachika mawili dakika ya 36 na 45 huku waliopindua meza kwa upande wa Simba walikuwa ni Betram Mombeki dakika ya 54, Joseph Owino (dk 58) na Gilbert Kaze dakika ya 85.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002